# MAANA YA USEMI NA MAZUNGUMZO KATIKA MITANDAO

# YA

# KIJAMII HUSUSANI FACEBOOK NA *TWITTER*

**KIUNGA MUKARIA TIMOTHY.**

**Tasnifu hii imetolewa ili kutosheleza baadhi ya mahitaji ya shahada ya Masters of Arts (Kiswahili) idara ya isimu na lugha Chuo Kikuu Cha Nairobi.**

**2016**

## IKIRARI

## MTAHINIWA

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijawahi kutolewa kutosheleza mahitaji ya shahada ya uzamili wa sanaa katika chuo kikuu chochote.

Sahihi……………………………Tarehe………………………………………….

Kiunga Mukaria Timothy.

(Mtahiniwa)

## WASIMAMIZI

Tasnifu hii imetolewa kwa madhumuni ya kutahiniwa kwa idhini yetu kama washauri na wasimamizi tulioteuliwa na Chuo.

Sahihi……………………………..Tarehe………………..

Dkt Tom Olali.

(Msimamizi)

Sahihi.......................................Tarehe……………………

Bw.Gitonga Josephat

(Msimamizi)

# TABARUKU

Kwa Marehemu babangu Kiunga Domiano M’Rukwaru aliyetuacha kabla ya kuona ndoto yangu ya masomo.

# YALIYOMO

MTAHINIWA ........ ii

TABARUKU ........ iii

YALIYOMO ........ iv

SHUKRANI ........ vi

SURA YA KWANZA ........ 1

1.0 UTANGULIZI ........ 1

1.1 TATIZO LA UTAFITI ........ 7

1.2 MADHUMUNI YA UTAFITI ........ 10

1.3 MSINGI WA NADHARIA ........ 11

1.5 SABABU ZA KUCHAGUA MADA ........ 16

1.6 UPEO NA MIPAKA ........ 18

1.7 YALIYOANDIKWA KUHUSU MADA ........ 19

1.8 MBINU ZA UTAFITI ........ 21

2.0 UTANGULIZI ........ 22

2.1.1 NYUMBANI ........ 22

2.1.2 UMBO ........ 23

2.1.3 UKUTA/KALENDA YA MATUKIO ........ 23

2.1.4 HALI ........ 24

2.1.5 TAARIFA ........ 24

2.1.6 SAMBAZA ........ 24

2.1.7 KIUNGO ........ 25

2.1.8 IMENIPENDEZA/HAINIPENDEZI ........ 26

2.1.10 RAFIKI ........ 29

2.1.11 TOKA NJE ........ 30

2.1.12 INGIA NDANI ........ 30

2.1.13 DOKOA/DUKUA ........ 30

2.1.14 BANDIKA/GADISHA ........ 31

2.1.15 PAKUA NA PAKIA ........ 31

2.2 MAELEZO YA VIJENZI MUHIMU VYA MADA NA UHUSIANO WAKE NA MITANDAO YA KIJAMII ........ 32

2.2.1 MAANA. ........ 32

2.2.2 USEMI ........ 34

2.2.3. MAZUNGUMZO ........ 36

SURA YA TATU ..... 47
3.0 SIFA ZA LUGHA YA MITANDAO YA KIJAMII KWA JUMLA ..... 47
3.1 MATUMIZI HOLELA YA LUGHA YA KISWAHILI ..... 47
3.2 KUCHANGANYA MSIMBO ..... 55
3.3 UFUPISHAJI WA MANENO KATIKA MITANDAO YA KIJMII ..... 58
3.4 USILABISHAJI KATIKA MITANDAO YA KIJAMII. ..... 62
3.5 LUGHA KATIKA MITANDAO YA KIJAMII INA SIFA ZA KIKONGAMANO AU MKUTANO DUARA ..... 66
3.6 MATUMIZI YA IKONIHISI NA PICHA ..... 68
3.8 UAKIFISHAJI KATIKA MITANDAO YA KIJAMII ..... 74
SURA YA NNE ..... 81
4.0. NAFASI YA MITANDAO YA KIJAMII KATIKA KULETA UTANGAMANO, NA KULEGEZA MIPAKA YA KITABAKA KATIKA JAMII ..... 81
4.1 HALI YA KUPUUZA KANUNI ZA USHIRIKIANO KATIKA MITANDAO YA KIJAMII ..... 83
SURA YA TANO ..... 99
5.0 TATHMINI NAMAPENDEKEZO ..... 99
5.1 MUHTASARI WA MATOKEO ..... 100
5.2 KUHUSU NADHARIA TETE ..... 100
5.3 MAPENDEKEZO ..... 102
MAREJELEO ..... 103
WOVUTI ZILIZOTEMBELEWA ..... 108

# SHUKRANI

Kwanza kabisa namshukuru Mungu kwa kunipa nguvu na kuniepusha na majanga pamoja na majaribu mengi ambayo yangenivuruga akili. Namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uwezo na subira ya kung'ang'ana na masomo haya hadi mwisho

Pili ningemshukuru kwa dhati mwalimu wangu wa awali, Mama Lucy Kamami Kiunga, kwa ushauri wake usiokoma, na bidii yake mithili ya mchwa kunilea hadi nimekuwa mtu mzima.Wahadhiri katika idara ya Kiswahili - Chuo Kikuu cha Nairobi wanastahiki shukrani si haba. Mchango wao wa moja kwa moja umenisaidia pakubwa katika kisomo changu. Wao ni Profesa. John Habwe, Dkt. P.I. Iribemwangi, Dkt. George Mweri, Dkt.Ayub Mukhwana na Profesa. K.W. Wamitila. Ushauri na maelekezo yao yamenifaa pakubwa, nashukuru.

Shukrani zangu maalum ni kwa wasimamizi wangu wawili; Dkt. Tom Olali na Bw. Gitonga Josephat. Mbali na kuwa walimu wangu, wasomi hawa walihusiana nami kama ndugu na sahibu mkubwa. Daima nitaishi kuwakumbuka kwa wema wao.

Ningependa vilevile kuwashukuru wafuatao: Maingi Cyprian, Ntika Jediel, Mwenda Laibuta, Joy Riungu, Mwendwa Purity, Jane Muema, Mutunga Ndereba, Ntongai Kirega, Jonah Muchena, Mugambi Gabriel na Edward Karithi. Wote hawa tuliofanya nao kazi katika shule ya upili ya Kilimamungu walinisaidia kwa njia moja au nyingine. Walinipa motisha hasa nilipoelekea kufa moyo. Nashukuru.

Ningependa vilevile kumshukuru mwalimu mkuu wa shule ya upili ya Kilimamungu kwa ukarimu wake kila nilipotaka likizo kwenda chuo kikuu cha Nairobi kushughulikia tasnifu hii.

Wenzangu tuliosoma nao wote wanastahili shukrani hasa marehemu Mukaria Reuben Muito, Mwende Alice, Maina Chege, Kavivi, Nickson na Otwere. Tulibadilishana nao mawazo kuhusu maswala ya kiusomi; bidii na uchangamvu wao vilinisaidia sana.

Tasnifu hii vilevile haingekamilika bila juhudi za rafiki na mpenzi wangu Stellah Kinya. Alivumilia upweke wa kutokuwepo kwangu wakati nilipokuwa nashughulikia tasnifu hii. Vilevile Ng'olua Titus, Jeremiah Tumbo, George Muroki, Issack Festus, Edward Karithi M, Douglus Ntongai, Rose Kabira, Peter Kabira na Janet Kerubo. Watu hawa wote kwa njia moja au nyingine walinisaidia kugharamia masomo yangu bila kinyongo.

# SURA YA KWANZA

## 1.0 UTANGULIZI

Mitandao ya kijamii ni tovuti au programu zinazowaruhusu watu kuungana na marafiki na familia na kushiriki taarifa, habari, picha, na video. Programu hizi huwasaidia watumiaji kuungana pamoja na kujipatia marafiki wapya na kuendelea kuwasiliana nao kwa kutumia mtandao wa intaneti. Kupitia mitandao hii watu hujenga mfumo wa mtandao wa marafiki ambao huweza kufikia maelfu na maelfu ya watu.

Mitandao ya kijamii ni uwanja ambao umeibuka kuwa na watumiaji wengi sana katika kipindi cha miaka michache iliyopita. Ni uwanja ambao umeibuka kuwa mashuhuri hasa baina ya vijana, wanasiasa na pia wanabiashara. Watumiaji wa mitandao ya kijamii huweza kujadili kuhusu maswala mbalimbali ya kijamii, kueleza kuhusu jambo fulani, kuwasiliana na kuuza au kununua bidhaa zao katika mtandao. Maendeleo ya kiteknolojia ndiyo hasa chanzo cha kutumika na kupanuka sana kwa mitandao ya kijamii. Maendeleo ya teknohama yamechangia katika kuzinduliwa kwa mitandao mingi ya kijamii.

Mitandao ya kijamii huhusisha lugha andishi ambayo kwa kiwango kikubwa huhusisha matumizi ya picha ili kupitisha ujumbe. Malengo ya mawasiliano katika mitandao ya kijamii huwa ni mengi. Lengo kuu la mawasiliano ni kuleta utangamano baina ya wanajamii. Kupitia mitandao ya kijamii watu huelewana kwa urahisi kwa sababu huwa wamejipanga katika makundi mbalimbali kwa mfano watu wanaofanya kazi pamoja, walio katika taaluma moja, waliosoma pamoja au wafuasi wa kikundi fulani mahususi kama vile kundi la kisiasa, kidini na kadhalika.

Mitandao ya kijamii huwa ni aina tu ya mawasiliano ya kielektroniki inayotumia kompyuta ambapo watumiaji au washiriki hujenga jamii ya kimtandao. Watumiaji hujenga urafiki katika mtandao na hivyo kushauriana, kujadiliana, kuliwazana na kadhalika katika mitandao. Hapa wanaweza kutumia maandishi, picha, sauti za kusikika na hata video. Utakuta kwamba watumiaji wa mitandao ya kijamii pamoja na kwamba ni ya kiutandawazi na inajumuisha watu wengi, watumiaji huweza kujigawa katika makundi pengine kulingana na walivyosoma, wanavyofanya kazi au wanatoka eneo moja kijiografia na hata kimbari na kuunda mfumo wa mtandao wa marafiki kama tulivyosema hapo awali.

Katika misingi hii ndipo watumiaji wake huweza kujitambulisha kupitia maneno ya msemaji. Maneno, sentensi na miundo mingine ya lugha inayotumika katika mitandao ya kijamii ni ya kipekee. Lugha katika mitandao ya kijamii haiwezi kutumika katika mazingira mengine. Angalia kauli ifuatayo kwa mfano ambayo ni maarufu katika mtandao wa *facebook*: *"Nairobi mimi hapa*!" Hapa msemaji anasema kuwa amefika mji wa Nairobi, inaweza kutumika katika mazingira hayo tu. Kupitia usemi huu tunajua kwamba msemaji hakuwa katika mji wa Nairobi na sasa tunapozungumza amefika mjini. Ili kushughulikia swala la mitandao ya kijamii kwa ukamilifu, tutachunguza historia ya mitandao hii kwa muhtasari.

Mawasiliano katika mitandao yalianza takriban miaka 40 iliyopita, ambapo barua pepe ya kwanza ilitumwa. Barua pepe ya kwanza ilitumwa kwa kutuma data baina ya tarakilishi mbili zilizokuwa zimewekwa mkabala kwa safu kupitia mtandao wa ARPANET, mtandao uliokuwa baadhi ya mitandao tangulizi ya mtandao wa intaneti.
. (http://www.mashable.com/2011/01/24/the-history-of social-media)

Hata hivyo historia ya mitandao ya kijamii ni changa mno. Inaweza kuangaliwa kuanzia mwaka wa 1994 ambapo mtandao wa kwanza wa kijamii ulizinduliwa. Mtandao huu *Geocities* ulilenga kuunganisha watu kutoka miji mbalimbali iliyokuwa na sifa fulani zilizofanana kwa mfano iliunganisha mji wa Hollywood na Wall Street ambayo ni miji iliyokuwa na sifa za kuwa maarufu katika maswala ya drama na maigizo ya kisanaa.

Mwaka wa 1997 shirika la huduma za kimtandao nchini Marekani (AOL-American online service) lilizindua huduma ya kutuma ujumbe wa moja kwa moja (instant messages) baina ya watu. Mtandao huu uliitwa ***degree.com***. Uliwawezesha watu kushirikiana kwa kutumiana picha, nyaraka na faili zingine ambazo huweza kutumwa kupitia mtandao huo hasa baina ya watu wanaofahamiana kama marafiki.

Kufikia mwaka wa 2000 kulitokea mwamko mpya katika matumizi ya mitandao ya kijamii na teknolojia kwa jumla. Jambo hili liliwasisimua watafiti wa mitandao ya kijamii na kuwapa motisha ya kuitafitia zaidi. Kutokana na juhudi zao mtandao wa *Friendster* ulizinduliwa ambao uliunganisha marafiki na kuwawezesha kutangamana na kuwasiliana kupitia ujumbe wa maandishi na picha. Matumizi ya *Friendster* yalipanda kufikia watumiaji milioni tatu kufikia mwaka 2002. Mtandao wa *Friendster* ulizua utanzu wake *my space* ambao ulipata matumizi mengi zaidi ya *Friendster*. Mtandao wa *My space* ulivuma hadi mwaka 2004 ambapo *facebook* ilizinduliwa. Awali mtandao wa *facebook* ulilenga kuwaunganisha wanafunzi wa chuo kikuu cha Havard Marekani. Tutaangalia historia ya *facebook* kwa mapana hapa chini.

Mwaka wa 2006 mtandao wa *twitter* ulizinduliwa. Mtandao wa *Twitter* ulipata watumiaji wengi zaidi na kuwa na umaarufu zaidi hasa wakati wa matukio yaliyo na umaarufu kama vile michuano ya kimataifa ya kandanda, raga au riadha(Kutoka http://esp.go.com/sport in social medi networks. Pamoja na kuwa mitandao ya kijamii ni mingi mno, mitandao ya *facebook* na *twitter* imeibuka kuwa na watumiaji wengi zaidi.

Katika utafiti wetu tutaangalia maana ya usemi na diskosi zinazopatikana katika mitandao ya kijamii. Hapa tutarejea mitandao ya *facebook* na *twitter* kama kesi stadi (uchunguzi kifani.) Kabla ya kuchambua mitandao hii ya kijamii tutaangalia historia ya mitandao ya *facebook* na *twitter.* Mtandao wa *Facebook* ulianzishwa na Mark Zuckenberg mwanafunzi wa Chuo kikuu cha Harvard pamoja na wanafunzi wenzake Eduardo Saverin, Chris Hughes na Dustin Moskovitz ikijulikana kama *thefacebook*. Neno *facebook* lilitokana na neno la kimsimu lililotumika sana katika Chuo cha Harvard kurejelea kitabu ambacho kilikuwa na pasipoti za wanafunzi wa chuo hicho pamoja na maelezo mengine yao kama vile majina na chumba cha kulala na kwa sababu hiyo kitabu chenyewe kiilitwa *face book*. *The* ilidondoshwa Juni, 2004 na kuwa na jina *facebook.* Zuckenberg pamoja na wanafunzi wengine walidakua wavuti wa idara ya mtandao katika Chuo kikuu cha Havard. Waliiba picha za wanafunzi wenzake pamoja na maelezo mengine ya kimsingi kama vile kitivo, jina, na kadhalika na kuziweka pamoja katika mtandao wao mpya. Picha hizi zilipata watazamaji wengi sana baada ya muda mchache tu (http://venturebeat.com/2008/12/18-history-and-growth-of-facebook. Juni mwaka wa 2004 makao makuu ya *facebook* yalihamishwa hadi Palo Alto Carlifornia. Kufikia Oktoba 2005, matumizi ya *facebook* yalikuwa yamepanuka na kuenea katika takriban vyuo vikuu 21 Uingereza na kuzindua aina

iliyoweza kutumika katika shule za upili. Baadaye *facebook* iliwaruhusu wafanya kazi wa kampuni mbalimbali kama vile *Microsoft* kujiunga na mtandao wa *facebook,* Hata hivyo kufikia mwaka 2006 *facebook* iliruhusu yeyote aliyefikia umri wa miaka 13 kujiunga na *facebook* bora awe na anwani ya barua pepe halali.

Mnamo Oktoba, 2008, mtandao wa *facebook* ulitangaza mpango wa kuhamisha makao yake makuu hadi Dublin, Ireland. Hadi 2010 *facebook* ilikuwa imepanuka kwa kiasi kikubwa zaidi. Februari, 2011 *facebook* iliibuka kuwa mtandao wenye matumizi mengi zaidi. Kufikia Aprili 2012, *facebook* ilikuwa na watumiaji takriban milioni mia tisa. Mtumiaji wa *facebook* anapoingia katika kivinjari cha kompyuta iliyounganishwa na intaneti, huchapa anwani au URL ya *facebook* ambayo ni http;//www.facebook.com huingia katika wavuti wa *facebook* ambapo anapaswa ama kuingia ikiwa ana akaunti katika mtandao wa *facebook* au kujisajili ikiwa mtumiaji hana akaunti. *Facebook* inapatikana katika takriban lugha sabini za ulimwengu ikiwemo lugha ya Kiswahili. Kuna eneo la kuingia katika ukurasa wa *facebook* kwa lugha ya Kiswahili ambapo msamiati maalum wa mtandao huu pamoja na msamiati wa kiteknolojia umetafsiriwa kwa mfano :

- Ingia-*log in*
- Nywlia-*Password*
- Toka nje-*Log out*
- Jisajili-*log up*

Kwa muhtasari ukurasa wa nyumbani (Ukurasa wa kwanza mtu anapofungua mtandao huu) wa *facebook* unatumia lugha ya Kiswahili. Makaribisho ni katika lugha ya Kiswahili kwa mfano mtumiaji huulizwa “Unafikiria nini?” au “sasisha hali yako,”

Hapa anatakiwa kuandika chochote kilicho akilini mwake hasa habari anazotaka ziwafikie watumiaji wengine. Mara nyingi anachoandika mtu hutegemea hali ya mazingira yake, yaani kinachotawala diskosi za wanajamii wakati huo kwa mfano siasa, michezo na kadhalika. Pamoja na kutumika kuleta utangamano mtandao wa *facebook* umetumikapia katika kueneza lugha ya Kiswahili kote ulimwenguni. Hata hivyo mtandao wa *facebook* umekashfiwa kwa kiwango kikubwa kuwa unasababisha uzoefu na kupoteza muda mwingi. Watumiaji hutawaliwa na matumizi yake kiasi kwamba wanatumia muda mwingi wa kufanya kazi katika mtandao huu wa *facebook*. Mtandao mwingine wa kijamii tutakaouchunguza ni mtandao wa *twitter*. Pia tutaangalia historia ya mtandao huu wa kijamii kabla hatujaanza kufanya uchambuzi wa maana ya usemi na mazungumzo kulingana na lengo letu.

Mtandao wa pili tutakaochunguza ni *twitter. Twitter* ni mtandao wa kijamii unaotoa huduma za kimikroblogi ambapo watumiaji hutuma ujumbe katika herufi zisizozidi 140. Mtandao huu wa kijamii ulianzishwa mnamo machi 2006 na Jack Dorsey na kuzinduliwa Julai mwaka huo huo. Dorsey alikuwa mwanakamati wabodi/halmashauri ya kampuni ya Podcasting Odeo. Walilenga kuutumia kupitisha ujumbe baina ya wafanya kazi wa kampuni (Memo za kampuni). Awali iliitwa *twttr* kisha kuingizwa irabu /i/ na /e/ kurahisisha matamshi yake. Kutoka kwa http://www.140characters.com/2009/01/30-how-twitter-was-born. Ujumbe unaotumwa katika *twitter* huitwa *tweet.* Kufikia mwaka wa 2011 idadi ya utumiaji wa *twitter* ilikuwa imefikia *tweet* milioni 140 kwa siku na kuwa nambari ya tatu baina ya mitandao ya kijamii. *Twitter* tofauti na *facebook* haijatumika katika lugha ya Kiswahili (Hadi tulipoandika kazi hii 2015) Msamiati unaotumika katika *twitter* haujatafsiriwa hadi katika lugha ya Kiswahili. Hata hivyo lugha ya Kiswahili

imeenezwa na kukuzwa kupitia *twitter*. Kuna kurasa katika mtandao wa *twitter* zinazohusu lugha ya Kiswahili kama vile @kiswahili books,@dw Kiswahili, @swahili sanifu na kadhalika. Pamoja na kurasa hizo zinazohusu lugha ya Kiswahili, kuna baadhi ya vyombo vya habari kama vile BBC Swahili, KTN Swahili, Taifa leo na kadhalika ambavyo huchapisha mtandaoni katika lugha ya Kiswahili. Kama ilivyo *facebook* matumizi ya *twitter* hupanda wakati wa matukio ya kimataifa au matukio yaliyo na wafuasi wengi kama vile michuano ya kadanda, mipira ya Raga, riadha na kadhalika. Mtandao wa *twitter* umeendelea kupanuka na kutumika katika mawanda mapana.

## 1.1 TATIZO LA UTAFITI

Mitandao ya kijamii ni mingi na inachukua miundo na kusheheni sifa mbalimbali kama tulivyoangalia hapo juu. Mazungumzo na semi zinazopatikana katika mitandao ya kijamii huwa na sifa za kipekee ambazo huwasaidia watumiaji kuelewana. Sifa hizi za kipekee katika mitandao ya kijamii hazijafanyiwa utafiti wowote. Sifa hizi ndizo zinazowaleta watumiaji wa mitandao ya kijamii pamoja na kuweza kuwasiliana hata kama wanatofautiana kiumri, kimaeneo na hata kihadhi katika jamii. Ingawa mitandao ya kijamii imetumika katika kuwazindua wanajamii kisiasa na kiuchumi kutokana na nguvu zake za kunasa hadhira kwa urahisi haijatafitiwa ipasavyo hasa katika misingi ya isimu. Sifa za lugha inayotumiwa katika mitandao ya kijamii hazijafanyiwa utafiti katika misingi ya kiisimu kwa jumla na hata katika misingi ya kiisimujamii. Vipengele vya kiisimujamii kama vile kuchanganya na kubadili msimbo, matumizi ya vifupisho au akronimu, matumizi ya sheng', kanuni za mawasiliano na kadhalika havijafanyiwa utafiti wowote. Hii ni kwa sababu vipengele

hivi hufanya kazi maalum katika mawasiliano ya mitandao ya kijamii, na huchangia sana katika kusaidia watu kuelewana.

Maswali kama vile: Je lugha katika mitandao ya kijamii ina sifa bainifu? Lugha ya Kiswahili hutumika vipi katika mitandao ya kijamii? Je watumiaji wa mitandao ya kijamii wanaweza kujiweka katika makundi mbalimbali kwa misingi ya lugha wanazotumia? Je kuna vipengele vyovyote vya kiisimu au kiisimujamii katika mitandao ya kijamii na vina nafasi gani katika kufanikisha mawasiliano? Je mtu anapotumia kiakifishi kama alama ya hisi hapa chini analenga kuonyesha hisia gani?




Ni dhahiri kuwa usemi huu hauhitaji kuandamana na alama za mdokezo lakini anazitumia. Je ,mbona shirika kubwa na la kuheshimika kama hili lipuuze kanuni za kisarufi za lugha ya Kiswahili na hakuna anayelalamika? Haya ni baadhi ya mambo yanayopatikana katika mitandao ya kijamii ambayo bado hayajafanyiwa utafiti. Kutoka kwa [www.facebook.com/KTNJameni](http://www.facebook.com/KTNJameni)

Si viakifishi tu ambavyo matumizi yake asilia yamebadilishwa. Mitandao ya kijamii imebadilisha vifupisho mbalimbali na watumiaji wake wamekubali mabadiliko hayo. Hata hivyo swala hili halijafanyiwa utafiti wowote wa kiisimu. Maswali haya na mengine mengi bila shaka hayajajibiwa. Hii ni kwa sababu hakuna utafiti uliofanyiwa lugha inayotumiwa katika mitandao ya kijamii. Haijafanyiwa utafiti wowote ambao unaangalia jinsi vipengele mbalimbali vya kiisimu na vya kiisimujamii vinavyochangia kuleta mawasiliano. Ni katika misingi hii utafiti wetu utalenga kuangalia sifa za lugha ya mitandao ya kijamii kama inavyotumika na mashabiki wake.

## 1.2 MADHUMUNI YA UTAFITI

Lengo kuu la utafiti huu ni kuangalia sifa za lugha ya mitandao ya kijamii. Tumelenga kuangalia jinsi vipengele mbalimbali vya kisarufi vinavyotumiwa ili kuleta maana katika mawasiliano. Pia jinsi msemaji anavyotumia maneno, picha, video na ishara mbalimbali kumaanisha jambo tofauti au kuleta maana tofauti na inayoweza kubebwa na maana ya vipashio katika sentensi au kauli hiyo.

Tutaangalia vilevile nafasi ya mafumbo au lugha fiche katika kuelewa anachomaanisha msemaji lakini la muhimu zaidi ni kuangalia nafasi ya chukulizi mbalimbali za msemaji na ikiwa chukulizi hizo zinamsaidia msikilizaji kuelewa kauli za msemaji. Katika mitandao ya kijamii kuna ukurasa wa nyumbani kwa mfano katika *facebook* au *twitter* mtumiaji huombwa kusasisha hali yake. Hapa mtumiaji huandika linalomsisimua au kutawala fikra zake wakati huo. Anapoandika marafiki wake au wafuasi wake hutoa maoni kuhusiana na anachoandika katika ukurasa huo wa nyumbani.

Tunaweza kuchambua hili kwa kuangalia maoni ya wasemaji kuhusiana na kauli ya msemaji kwa mfano mtumiaji wa *facebook* au *twitter* anaposasisha hali yake katika ukurasa wa nyumbani wa *facebook* au *twitter* mara nyingi watumiaji wengine wa mitandao hii wanapotoa maoni huwa yanalenga au kukosa kulenga alichomaanisha mwandishi wa kauli. Tutajiuliza, "Je ni jambo gani huchangia katika kuelewa au kutoelewa kauli ya mwandishi au kilichokuwa akilini mwake. Je wanaafikiana na kauli ya msemaji? Mara nyingi ikiwa anachomaanisha msemaji hakieleweki basi hakuna mawasiliano mwafaka. Pia huenda kukakosa yeyote anayeonyesha hisia zozote kuhusiana na kilichoandikwa. Nafasi ya muktadha, wakati na matukio mbalimbali ya kitaifa au kimataifa pia yatachangia pakubwa katika kuelewa maana ya semi katika mitandao ya kijamii. Pia tutaangalia nafasi ya kubadili na kuchanganya msimbo, matumizi holela ya lugha ya Kiswahili na hali ya kupuuza kanuni za ushirikiano za **Grice (1975**) katika mitandao ya kijamii.

## 1.3 MSINGI WA NADHARIA

Utafiti wetu utajikita katika nadharia ya umaanisho ya **Grice(Gricean implicalture theory)**. Nadharia hii iliasisiwa na H.P.Grice. Kulingana na Grice, kuna aina mbili za maana katika usemi au kauli yoyote. Maana hizi ni maana ya lugha na maana ya msemaji. Maana ya lugha ni maana inayotokana na vipashio vya sentensi ilhali maana ya msemaji ni maana inayoibuka kutokana na matumizi ya maneno hayo katika sentensi.

Nadharia ya umaanisho imekuwa nadharia muhimu sana katika tawi la isimu. Hii ni kwa sababu pragmatiki hulenga maana kulingana na msemaji na umaanisho

hushughulikia maana inayojitokeza kutokana na maneno ya msemaji. Grice anasema kuwa msemaji husema au hutoa maana ambayo haijitokezi katika vipashio vya kisarufi kama vile maana za maneno katika sentensi. Kwa mfano katika mazungumzo haya, jibu la (b) halikubaliani na swali la msemaji.

a) Nipe kalamu.

b) Nimepoteza funguo.

Tukirejelea mazungumzo hapo juu, ikiwa (a) atauliza, “Kwa nini hujafungua dawati?” Jibu litakuwa lile lile lakini wakati huo ikiwa na maana tofauti. Hivyo msemaji huweza kumaanisha mambo mengine tofauti na anavyosema ama kulingana na muktadha au maneno katika sentensi hizo.

Levinson S.C. (1983) anasema kuwa umaanisho ni nadharia inayoonyesha kwamba kuna uwezo wa kumaanisha jambo tofauti na linalosemwa katika sentensi (jambo tofauti na linalobebwa na maneno katika sentensi hiyo). Katika lugha ya Kiingereza.

1. Is it lunch time?

2. The food is in table room

Katika mazungumzo haya kinachosemwa na 2 hakihusiani na swali la 1 lakini 2 amejibu swali la 1.Tunatarajia kwamba 2 angesema ndio au la. Umaanisho ni nadharia ambayo ni changa mno. Hoja muhimu kuhusiana na nadharia hii zilipendekezwa na William James mhadhiri katika Chuo kikuu cha Harvard mwaka wa 1967 na kuchapishwa na Grice mwaka wa 1975. Grice alitoa kanuni nne kuu ambazo aliamini kuwa muhimu katika mawasiliano.

Kulingana na Grice (1975) maana hupatikana kutokana na ushirikiano baina ya wasemaji na wasikilizaji. Ni katika ushirikiano huu ambapo msikilizaji huweza

kutambua kwa nini msemaji anasema anachosema na analenga nini kwa kusema hivyo. Alitoa kanuni nne ambazo zinahitaji kufuatwa ili kuelewana baina ya msemaji na msikilizaji. Kanuni hizi ni:

**1. Kanuni ya idadi.**

Kusema yanayotosheleza unachosema bila kuzidi kiasi chako. Usizidi wala kupunguza taarifa kuhusiana na mada. Anasisitiza kutoa taarifa inayotosheleza mada inayozungumziwa.

2. **Kanuni ya namna**.

Kutotumia mafumbo na lugha fiche katika usemi. Lugha ieleweke na wasikilizaji/walengwa bila utata wowote. Mchango uwasilishwe kwa njia iliyo dhahiri. Pia linalosemwa lisemwe kwa utaratibu unaoeleweka. Kanuni hii pia inahimiza kutumia lugha inayovutia wasikilizaji au walengwa (isiyochosha), msemaji aseme kwa njia dhahiri na isiyomsumbua mlengwa kuielewa.

**3. Kanuni ya uhusiano.**

Sema kinachohusu mada yako. Jikite katika muktadha wa usemaji au mazungumzo, toa hoja ambazo zinahusu mada ya mazungumzo.

**4. Kanuni ya ukweli.**

Sema kile ambacho unaweza kudhibitisha. Usiseme ambacho unajua si kweli. Mchango wako uwe na ukweli unaoweza kudhibitika.

Grice aliita kanuni hizi za ushirikiano na kulingana na Grice msemaji huweza kuvunja au kupuuza kanuni hizi kwa namna moja au nyingine. Uvunjaji au upuuzaji huu wa kanuni huweza kusababisha umaanisho katika mazungumzo. Angalia mazungumzo yafuatayo baina ya mwanafunzi a na b:

a. Mwalimu ameenda nyumbani?

b. Silioni gari lake.

Katika mazungumzo haya,b anapuuza kanuni ya idadi na vilevile ya uhusiano. Hata hivyo analeta maana kwamba pengine b hana uhakika kama mwalimu aliendа au yupo lakini anamaanisha kwamba pengine aliendа kwa sababu gari lake halionekani na hulitumia kutoka nje ya shule au kwenda nyumbani.

Habwe na Karanja (2004) wakiwanukuu Leech 1983 na Searle 1969 wanasema kuwa wakati wa kuzungumza wasemaji hawaelezei mambo fulani kwa uwazi hali inayopelekea umaanishaji katika maana. Kulingana na Grice 1975 sababu kuu ya umaanisho ni kupuuzwa kwa kanuni za ushirikiano. Kanuni yoyote inapopuuzwa husababisha umaanisho hata hivyo wazungumzaji huelewana kwa sababu ya muktadha. Kwa mfano katika mazingira ya shule ambapo wanafunzi hawaruhusiwi kubeba vitu fulani shuleni kisha mwalimu amwite mwanafunzi aliyebeba mkoba kuchunguza ikiwa ana bidhaa zozote haramu kwa mkoba wake tunaweza kupata mazungumzo ya aina hii.

Mwalimu: Halima, kuna nini ndani ya mkoba huo?

Mwanafunzi: Samahani mwalimu, hamna chochote.

Mwalimu: Ulete mkoba niukague (Anaukagua na kisha anamruhusu mwanafunzi kwenda darasani)

Mwanafunzi: Asante mwalimu (Anaenda zake)

Levinson S.C (1983) anasema kuwa katika mazungumzo ya kawaida kanuni za ushirikiano za Grice za hazizingatiwi katika ujumla wake. Hata hivyo wasikilizaji huchukulia kwamba msemaji anashirikiana. Katika mazungumzo ya mwanafunzi na mwalimu hapo juu; mwanafunzi anapoulizwa amebeba nini mkobani anadai kuwa

hamna ilhali mkoba umejaa vitabu, nguo, na vitu viingine vya matumizi shuleni. Hata hivyo mwalimu anaelewa anachosema kuwa hajabeba bidhaa haramu shuleni. Kulingana na Levinson mwanafunzi anavunja kanuni ya ukweli lakini mwalimu anamwelewa kwa sababu ya muktadha na elimu shirikishi.

Levinson S.C (1983) anasema kuwa ingawa mara nyingi kanuni za ushirikiano za Grice hazizingatiwi kabisa katika kila mazungumzo, msikilizaji huchukulia kuwa msemaji anashirikiana kulingana na muktadha.

Mawazo haya yanaungwa mkono na Marimaridou Sophia S.C (1983) anayesema kuwa, ingawa mara nyingi wazungumzaji hukosa kuzingatia kanuni za ushirikiano za Grice msikilizaji huchukulia kuwa kununi zimezingatiwa. Marimaridou anatoa mfano ufuatao wa mazungumzo kwa lugha ya Kiingereza baina wa wasemaji A na B:

A: Has Helen come yet?

B: The computer is on.

Anasema kuwa ikiwa jibu la B litachukuliwa kijuujuu basi itaonekana kuwa B anabadili mada inayojadiliwa kwa kuwa haionekani kuzingatia kanuni ya Grice ya uhusiano. Hata hivyo msikilizaji anapata maana kwa msingi kuwa anashirikiana.

Kulingana na maoni haya tunaweza kusema kuwa kanuni za ushirikiano za Grice si sheria zinazoelekeza jinsi mazungumzo yanavyopaswa kuendeshwa ambazo ni lazima zijidhihirishe katika kila mazungumzo.

## 1.4 NADHARIA TETE

Utafiti wetu umetekelezwa katika misingi ya nadharia tete zifuatazo;

1. Lugha ya mitandao ya kijamii huwa na sifa maalum ambazo huipa upekee fulani unaochangia katika kutekeleza majukumu yake.
2. Lazima muktadha wa usemaji ueleweke ili kupata maana ya kauli au chapisho za mitandao ya kijamii.
3. Aidha tumechukulia kwamba diskosi katika mitandao ya kijamii hufanana kabisa na mazungumzo ya ana kwa ana.

## 1.5 SABABU ZA KUCHAGUA MADA

Mitandao ya kijamii imetumiwa na watu wenye umri, matabaka na hadhi tofautitofauti. Tangu ilipoanza duniani blogu kadha zinazohusu nyanja mbalimbali za binadamu zimechapishwa mtandaoni. Lugha katika blogu hizi imekuwa ikiteka nadhari zangu kwa muda mrefu. Katika mitandao ya kijamii niliangalia lugha inayopatikana huko na kujaribu kuichanganua. Mambo kadha yalinisumbua hasa namna watumiaji wanavyochagua lugha inayotumika. Mambo kama vile uteuzi wa silabi, miundo ya maneno na sentensi yalinisumbua sana. Hapa chini ni sasisho la mtumiaji wa mtandao wa *facebook* ambalo limeandikwa kwa lugha ya Kiingereza kama lugha asilia. Hata hivyo miundo ya sentensi katika usemi huu ina mambo mengi ambayo yanahitaji kuchunguzwa kiisimu na kiisimujamii, utafiti huo haujafanywa kwa hiyo, ikawa sababu moja ya kuchagua mada hii ili kuweka wazi sifa za sajili hii mpya.


Veacqueyteatar Shqqeenaj

**Nachukia ninavyojihisi…..Namkosa mtu fulani ambaye sifahamu kama yuanikosa pia…Nahitaji mungu anisaidie haraka iwezekanavyo.**

Imenipendeza · · Sambaza · Dakika 23 zilizopitavia (kupitia) rununu: ·

- Tracy Bridget Wamuyu amependezwa na hii.

  - 


    Veacqueyteatar Shqqeenaj hahahaha...bro!msm..utawezana qweli..unless u qam arnd n do e tokin...(Kicheko…kaka nimekukosa…utayaweza kweli? …pengine uje tuzungumze)

    Dakika 7 zilizopita via (kupitia)rununu · Imenipendeza

  - 

    Calvin Njays Ata ukimtxt ananga risto as u expct.bad.really bad (Hata ukimtumia ujumbe mfupi hajibu kama ninavyotarajia.Hiyo ni hali mbaya)

    dakika moja iliyopita via (kupitia)rununu · Imenipendeza




(Kutoka http://www.facebook.com/Veacqueyteatar Shqqeena)

Ukiangalia mazungumzo haya utagundua sifa ambazo hazijazoeleka katika lugha sanifu na ambazo zitahitaji mtu kuwa na uelewa fulani ili kupata maana yake. Baadhi ya sifa hizi ni pamoja na matumizi tofauti ya alama za kuakifisha kama vile alama za dukuduku, vifupisho kama vile ASAP, matumizi ya sauti kusimamia neno, sifa ambayo ni maarufu sana katika mitandao ya kijamii kwa mfano /*u*/ kusimamia *you.*

Mambo haya na mengine mengi hayajafanyiwa utafiti na kuwekwa bayana kwa wanaisimu ili kuwa na pa kurejelea. Hii pia ikawa sababu yetu kuu ya kuchagua mada ambapo tunatarajia kuibuka na mambo kadha mapya ambayo yatakuwa na

umuhimu katika usomaji wa isimu. Ieleweke kuwa, mitandao ya kijamii ni mipya na imeingia na daima itakuwa sehemu ya maisha ya wanadamu kwa hiyo lugha yake isipofanyiwa utafiti na kuwekwa wazi basi kutakuwa na pengo kubwa katika isimujamii.

Uvumbuzi wa vifaa vya teknolojia ya mawasiliano kama vile vipakatalishi, ipad, na kadhalika vimechangia sana katika kukua kwa mitandao ya kijamii. Kwa mfano mtu anaposafiri garini ana*face*buku,ana*tweet* na kadhalika. Msamiati bila shaka umeibuka ambapo mwingi umetokana na maneno ambayo tayari yana maana nyingine lakini yanapewa maana tofauti kurejelea swala tofauti katika mitandao ya kijamii.

Kaida fulani zimeibuka na kukubalika baina ya watumiaji wa mitandao ya kijamii ambazo bila shaka zinajenga aina fulani ya sajili. Sajili hii ambayo tutaiita sajili ya mitandao ya kijamii haijafanyiwa utafiti kama vile sajili nyingine zilivyofanyiwa utafiti na kuwekwa wazi. Mada hii italenga kuangalia sifa za lugha katika mitandao ya kijamii kama sajili inayojisimamia na yenye sifa zake bainifu. Uchunguzi huu kwa muhtasari utakuwa umeendeleza utafiti wa kiisimujamii na kipragmatiki na kwa hiyo utakuwa mchango mkubwa kwa isimu kwa jumla.

## 1.6 UPEO NA MIPAKA

Mitandao ya kijamii ni mingi kwa mfano kuna *facebook, Twitter, bebo, Friendster, hi5, myspace, misik, flixster, bebo,whatsApp*na kadhalika. Hata hivyo katika utafiti wetu tutarejelea mitandao miwili tu ya kijamii ambayo ni *facebook* na *twitter,* mitandao inayotumika sana. Tutarejelea maana ya kipragmatiki bila kujikita katika maudhui yanayopatikana katika mitandao hii pamoja na vipengele viingine vya

kisarufi. Tutaangalia maana kama ilivyodhamiriwa na msemaji. Pia katika kukusanya na kuchanganua data inayopatikana katika mitandao ya *facebook* na *twitter* tutatalii maandishi yaliyowekwa katika mitandao kutoka mwaka wa 2010 hadi Juni 2015. Tutachunguza diskosi katika kurasa za watumiaji kadhaa wa *facebook* na *twitter* katika miaka mitano iliyopita lakini tutaangalia miezi ambayo huwa na shughuli nyingi kama vile wakati wa Krismasi, mwezi mtukufu wa Ramadhani ama wakati wa uchaguzi mkuu. Maudhui katika mitandao ya kijamii huwa chungu nzima. Hata hivyo hatutashughulikia maudhui katika mitandao ya kijamii.

## 1.7 YALIYOANDIKWA KUHUSU MADA

Swala la mitandao ya kijamii halijashughulikiwa sana katika isimu. Mwaringa .D .K (2002) ameshughulikia swala la mitandao ya kijamii katika mada "**Globalization and cultural impact of the media**: **A web analysis of the facebook social network.**" Maina W.Rachel anaangalia jinsi lugha ya Kiswahili inavyotumika katika mitandao ndani ya makala **Kiswahili kwenye mtandao** katika Chimerah Rocha na wengine (2011) (ed) **Kiswahili research anddevelopment in Eastern Africa**. Shawcroft S. R (2014) **Gender differences in texts messaging**: Brigham Young University, Ameangalia namna jinsia inavyoathiri matumizi ya lugha katika ujumbe mfupi wa simu. Shawcroft anasemakuwa ujumbe mfupi wa simu umeathiri sana namna vijana wa Marekani wanavyotumia lugha ya Kiingereza.

Mohammed Nunuu Abdullah (2013) katika tasnifu yake anaangalia athari za lugha tandawazi katika simu za kiganjani. Mohammed anasema kuwa simu za kiganjani zimeathiri namna watu wanavyozungumza kwa kutumia lugha ya Kiswahili.

Anasema kuwa lugha ya Kiswahili imebadilishwa na simu za mikononi kwa kiwango kikubwa.

Mutembei (2011) naye katika tasnifu yake ya uzamili iliyowasilishwa chuo kikuu cha Kenyatta, aliangalia matumizi ya simu za mkononi katika mawasiliano. Alishughulikia matumizi ya simu za mkononi katika kuandika ujumbe mfupi. Kulingana na Mutembei, ujumbe mfupi wa simu umerahisisha mawasiliano. Hata hivyo anasema kuwa ujumbe mfupi wa simu umevuruga matumizi na sarufi ya lugha ya Kiswahili kwa kiwango kikubwa. Mutembei na Nunuu wanaiita sajili tandawazi. Hata hivyo sajili hii inaweza kujitokeza zaidi katika mitandao ya kijamii.

Taga Caroline (2009) pia katika tasnifu yake ya uzamifu **Acopus linguistics study of sms texts messaging** iliyowasilishwa katika chuo kikuu cha Birmingham anasema kuwa kuna mshabaha kubwa baina ya lugha ya ujumbe mfupi wa simu na lugha ya mitandao. Taga anasema kuwa matumizi ya simu za mkononi hutawaliwa na matumizi ya vifupisho, akronimu na matumizi ya nambari baina ya maneno sifa ambayo hujitokeza sana katika lugha ya mitandao.

Mohammed M. R (2012) anasema kuwa kuna mfanano mkubwa baina ya lugha ya barua pepe na lugha ya mazungumzo ya kawaida. Mohammed anaiita lugha ya mitandaoni kama vile ya barua pepe teknousemi.

Danet Brenda (2002) anaangalia sifa za lugha ya barua pepe ingawa anasema kuwa uchunguzi wa barua pepe una changamoto nyingi kwa kuwa mazungumzo ya barua pepe ni ya kifaragha na watu huitumia katika mazungumzo yanayohusu shughuli za

kibinafsi. Kutokana na sababu hiyo inakuwa vigumu kupata data mtafiti anapochunguza au kutafiti barua pepe na ujumbe mfupi.

Hawa wote hawajashughulikia maana ya diskosi katika mitandao ya kijamii hasa namna lugha ya Kiswahili inavyotumiwa katika mitandao hii .

## 1.8 MBINU ZA UTAFITI

Sehemu kubwa ya utafiti wetu itakuwa intaneti ambapo tutadurusu aina zozote za matini

ambazo zitakuwa za manufaa kama vile vitabu, tasnifu na gazeti hasa la *Taifa leo* linalochapishiwa nchini Kenya. Pia tutatembelea kurasa za watangazaji wa mashirika yanayochapisha habari katika mtandao wa *facebook* na *twitter*. Hapa tutaangalia makala mtandaoni pamoja na makala zilizopigwa chapa. Mitandao ya kijamii pia itakuwa muhimu katika utafiti wetu. Tutatalii kurasa za watumiaji mbalimbali wa *facebook* na *twitter* kisha kuchanganua data tutakayoipata.

Pia tutadurusu aina zozote za matini ambazo zitakuwa za manufaa kama vile vitabu vilivyochapishwa na tasnifu ambazo hazijachapishwa katika maktaba mbalimbali za vyuo vikuu.

Tutawarejelea wataalam mbalimbali katika uwanja huu wakiwemo waandishi na watangazaji wa habari. Ili kuona jinsi mitandao ya kijamii inavyotumika katika kupasha habari, tutawahoji watangazaji katika runinga ya KTN nchini Kenya, mtangazaji mmoja kutoka redio Citizen inayomilikiwa na *Royal media services* ambayo ni kampuni ya Kenya, vilevile na mhariri mmoja wa gazeti la *Taifa leo* linalochapishiwa nchini Kenya. Kila tutakayemhoji au mitandao tutakayoshughulikia ni ile inayotumia lugha ya Kiswahili. Uchanganuzi wetu wa lugha ya mitandao ya kijamii utakuwa wa kiuelezi pamoja na matumizi ya takwimu.

# SURA YA PILI

## 2.0 UTANGULIZI

Watumiaji wa mitandao ya kijamii wameibua istilahi mbalimbali ambazo zinachangia katika mawasiliano yanayohusiana na mitandao ya kijamii. Istilahi hizi huwa na maana ambazo huweza kueleweka katika muktadha wa mitandao ya kijamii pekee. Mikakati ya kipragmatiki hutumika kuibua istilahi hizi ambazo huwa na maana ya umaanisho. Nadharia ya Grice ya umaanisho itakuwa muhimu katika uchanganuzi wa istilahi katika mitandao ya kijamii. Hata hivyo ni msamiati unaopatikana katika lugha mbalimbali ambao huchotwa na kupewa maana mahususi inayojikita katika matumizi ya mitandao ya kijamii. Katika sehemu hii tutafafanua istilahi ambazo zimetafsiriwa hadi katika lugha ya Kiswahili.

## 2.1 UFAFANUZI WA ISTILAHI MUHIMU KATIKA MITANDAO YA KIJAMII

### 2.1.1 NYUMBANI

Ni tafsiri ya neno la Kiingereza "*home"* lakini haina maana sawa na maana asilia ya neno hili. Katika mitandao ya *facebook* na *twitter* neno hili hurejelea ukurasa wa kwanza katika mitandao hii. Mtumiaji wa mitandao hii anapoingia katika mtandao kwa kutumia ama namba ya simu au barua pepe pamoja na neno lake la siri/nywila sehemu anayojikuta huitwa nyumbani. Muundo wa neno hili unafanana na muundo wake katika lugha ya Kiingereza (home). Patzel M (2005) anaiita hali hii ya uundaji msamiati ukopaji sogeza ambapo muundo wa neno linalokopwa hufanana na muundo wa neno hilo katika lugha lengwa ingawa maana yake huwa na mabadiliko madogo.

Katika hali hii maana pia hukopwa kwa mfano katika mitandao kuna *Home page* kwa lugha ya Kiingereza. Neno hili kwa lugha ya Kiingereza hukopwa pamoja na maana yake na kuwa ukurasa wa nyumbani. Katika teknolojia ya mawasiliano *Home page* ni ukurasa wa kwanza katika wavuti. Kila wavuti una ukurasa wa nyumbani. Katika mtandao wa *facebook* au *twitter* ukurasa huu huitwa nyumbani. Unapochapa anwani ya mitandao hii ya kijamii katika kivinjari cha tarakilishi yako au katika injini tafuti ya wavuti unaotumia, ukurasa unaopata ni ukurasa wa nyumbani. Pia kuna baadhi ya mitandao ya kijamii kama vile *facebook, twitter, google+, youtube* na kadhalika ambayo huwa katika vifaa vya simu za mikononi kama mojawapo ya programu za wavuti. Hii ina maana kwamba unapotumia simu za mkononi hasa zile za *android* hauhitaji kutumia kivinjari chochote unaingia moja kwa moja na ukurasa unaokuta ni ukurasa wa nyumbani.

### 2.1.2 UMBO

Huu ni ukurasa wa pili katika mitandao ya *facebook* na *twitter* ambao huwa na maelezo kuhusu mtumiaji wa mitandao hii. Ni tafsiri ya neno la kiingereza *profile* katika mtandao wa *twitter* halijatafsiriwa. Katika ukurasa huu kuna maelezo mafupi kuhusu mtumiaji kama vile alikosomea,anapofanya kazi, jinsia yake, picha yake, barua pepe, anwani ya posta, mahali alikozaliwa,anapoishi na hata tarehe ya kuzaliwa. Maelezo haya mtumiaji huweza kuyahariri kwa kubonyeza tu nyuga za umbo ambazo huwa upande wa kushoto wa ukurasa huu.

### 2.1.3 UKUTA/KALENDA YA MATUKIO

Ni sehemu katika umbo la mtumiaji wa *facebook* au *twitter*. Hapa rafiki wa mtumiaji wa *facebook* au *follower* katika *twitter* huweza kutuma habari zozote kwa mfano kumuarifu kuhusu jambo fulani, kumualika katika shughuli fulani, kushauri na kutoa

habari zingine zenye umuhimu kama vile kutakia heri njema. Ni tafsiri ya neno la Kiingereza "*wall*". Ukuta ni mfano wa ubao wa matangazo katika mitandao ya kijamii. Hii ni kwa sababu ujumbe unaomlenga mtumiaji wa *facebook* huachwa au huandikwa hapa.

### 2.1.4 HALI

Kinachoandikwa na mtumiaji katika ukurasa wake wa nyumbani wa *facebook* au *twitter*. Ni tafsiri ya neno la Kiingereza "*status*" Huitwa hali kwa sababu mtumiaji hueleza jinsi mambo yalivyo kwa upande wake hasa anavyofikiria wakati huo. Kuandika jambo jipya katika nafasi ya hali huitwa kusasisha hali na huelekezwa na kauli hizi katika ukurasa wa nyumbani wa mitandao ya *facebook* na *twitter:*

"Unafikiria nini?" (*What is in your mind?)*-Swali.

"Sasisha hali yako" (*Update your status)* -Maelekezo.

Hali katika mtandao wa *twitte*r haijatafsiriwa huwa ni *tweet* maoni yanayotolewa huitwa *retweet.* Pia huitwa kipachiko katika mtandao wa *facebook*.

### 2.1.5 TAARIFA

Limetafsiriwa kutoka kwa "*notification*" tafsiri ambayo ni makosa kwa sababu neno sahihi hapa lingekuwa taarifu kwa sababu sehemu hii humuarifu mtumiaji wa mitandao kuwa kuna jambo fulani lililoendelea au lililotendeka katika ukurasa wake kama vile kutolewa maoni kwa hali yake ama habari zozote muhimu katika ukuta wake.

### 2.1.6 SAMBAZA

Ni tafsiri ya neno la Kiingereza "*share*". Kusambaza katika mitandao ya *facebook* na *tweeter* ni kueneza hali yako katika kuta za watumiaji wengine wa mitandao hii.

Lazima huidhinishe hadhira inayolengwa na tangazo hilo kama vile marafiki, au katika kundi fulani la watu. Mtu huweza kusambaza hali, kipachiko, au kiungo




### 2.1.7 KIUNGO

Kiungo hutumika kwa maana sawa na hali lakini huitwa hivi ikiwa kuna picha,video,au maandishi yanayowasilishwa kwa njia ya dosa umeme kama ifuatayo kutoka ukurasa wa Vituko VYA Zanzibar. Kikundi hiki cha watumiaji kilisambaza kiungo kilichobeba habari za rais wa Jamhuri ya Tanzania.




### 2.1.8 IMENIPENDEZA/HAINIPENDEZI

Maneno haya hutumiwa kwa maana ya kuafikiana, kufurahishwa au kupendezwa na kiungo au hali katika umbo la mtumiaji wa *facebook* au *twitter*. Maneno haya ni vitenzi. Kitenzi cha pili ni kikanushi cha kitenzi imenipendeza. Sifa moja kuu katika mitandao ya kijamii ni kuwa vinyume vya tendo fulani huwakilishwa na vikanushi.

Kwa sababu hii sasisho, picha au kiungo chochote ambacho hakikupendezi haina maana kuwa unakichukia. Maana inayowasilishwa na istilahi hii(hainipendezi) ni kuwa huna la kusema kuhusiana na jambo hilo. Ikiwa watumiaji watapenda hali ya mtumiaji wa *facebook* basi ukurasa utaonyesha idadi yao moja kwa moja. Ishara ya kidole gumba itatumika kuonyesha hali hii. Katika chapisho hili watu sabini na tano wanapendezwa na hali au sasisho la Vituko VYA Zanzibar. Katika ukurasa wa 30.




2.1.9. TOA MAONI

Kueleza hisia zako kuhusiana na hali au kiungo. Mara nyingi watumiaji wa mitandao ya kijamii husasisha hali kwa kutoa kauli ambazo zinazua mijadala hasa kuhusiana na maswala ya kijamii, kisiasa au kiuchumi. Mijadala hiyo hujadiliwa kwa kutoa maoni kwa njia ya maandishi. Ni sawa na kuchangia mjadala katika mazungumzo ya ana kwa ana. Angalia hali ifuatayo ya mtumiaji wa *facebook* ambayo inahusu sifa tofauti za wanawake kutoka Marekani,Uropa na Kenya ya Afrika. Kutoka @joehills katika http://www.facebook.com/joehills.

**Joehills Espinoz Githaiga**

**ukitaka kumtisha mwanamke wa USA mwambie una ukimwi, wa EUROPE(Uropa) cancer (saratani) na wa KENYA mwambie huna pesa .**

Dakika 28 zilizopita




sehemu hii huandikwa maoni ya wasomaji kuhusiana na hali hiyo.

Vilevile angalia hali ifuatayo katika ukuta/ukurasa wa Gazeti la Taifa leo ambayo imetolewa maoni na mashabiki wa jarida hilo. Maoni ya marafiki zake inatarajiwa yatalenga na kuhusiana na anachokisema ambacho ni kinyang'anyiro baina ya timu ya Chelsea na West Ham.

**GAZETI LA TAIFA LEO**
Chelsea yakabiliana na West Ham
26 Disemba 2014 · Hadharani · katika Picha za Kalenda ya Matukio
Tambulisha Picha · Tazama Ukubwa Kamili · Tuma kama Ujumbe · Ripoti

3

Andika maoni...

[ ] Toa maoni

Taja Marafiki

Bottom of Form

Yaya Bin Abdalah

Bilashaka( Bila shaka)

Poa · Jibu · Ripoti · 26 Disemba 2014

Hon Simon Nyongesa

lasima ita win kama kawaa (Lazima itashinda)

Poa · Jibu · Ripoti · 26 Disemba 2014

Pancwise Gamgee Kabisa!@ Hon Simon Nyongesa

Poa · Jibu · Ripoti · 26 Disemba 2014

Katika kutoa maoni, watu wengi huweza kuchangia na kujibizana papo kwa papo. Kwa hiyo unapojibu rafiki au mfuasi au unapotoa kauli inayoelekezwa kwa mtu mahususi na si wote wanaoshiriki katika kutoa maoni kwa hali ya mtumiaji wa mtandao huu, alama @ (kwa) hutumiwa kabla ya kutaja mlengwa kwa mfano @hon nyongesa hapo juu. Tutajadili zaidi kuhusu alama hii katika sura ya nne.

### 2.1.10 RAFIKI

Rafiki katika *facebook,na* mfuasi (*follower*), Katika *twitter*. Huyu ni mtumiaji wa mitandao hii ambaye ameidhinishwa na mtumiaji mwingine wa ukurasa fulani wa *facebook* au *twitter* kushirikiana na kutangamana naye katika mitandao hii. Rafiki huweza kutoa maoni kuhusiana na hali au kiungo cha mtumiaji mwingine. Kwa kuwa mitandao ya kijamii ni mahali au uwanja wa utangamano, hawa huwa ni watu ambao mtu huweza kutangamana na kuwasiliana nao katika ulimwengu wa mitandao ya kijamii. Watu mbalimbali huweza kuwa na marafiki wengi kulingana na umaarufu wao kwa mfano wanamuziki au wanasiasa huwa na idadi kubwa sana ya wafuasi au

marafiki kwa mfano rais wa Nigeria (2010-2015) Goodluck Jonathan mwaka wa 2011 alikuwa na marafiki wengi zaidi ya jumla ya marafiki wa waziri mkuu wa Uingereza David Cameron, Chancela wa Ujerumani Angela Markel na Rais wa Afrika kusini Jacob Zuma wakiwa pamoja. Hii ni kwa sababu ya tabia na hulka yake njema kuhusiana na mitandao ya kijamii. (http://www.cp.Africa.com/presdent-goodluck@cpafrica )

Msamiati unaohusiana na istilahi Rafiki au Mfuasi katika mitandao ya kijamii

***FacebookTwittterMaana***

- *Friend* *Follower* Rafiki katika mitandao hii mnaweza kutangamana naye.
- *Add friend* *Follow* Mjumlishe rafiki au mfanye rafiki.
- *Unfriend* *Unfollow* Ondoa urafiki.

### 2.1.11 TOKA NJE

Funga ukurasa wako wa *Facebook* au *Twitter*.Ni tafsiri ya neno "log out" au "Sign out."

### 2.1.12 INGIA NDANI

Kuingia katika mtandao na kuanza kuwasiliana. Kuingia lazima au mtu huhitajika kuwa na barua pepe inayotumika, namba ya simu au jina la utumiaji pamoja na haya lazima hawe na nywila au neno la siri ambalo analifahamu yeye mwenyewe ili kuakikisha usalama na faragha ya akaunti yake. Hii ni tafsiri ya "log in" au "sign in".

### 2.1.13 DOKOA/DUKUA

Kuashiria mtu kwa kutumia kidole. Huwa ishara ya kuonyesha rafiki au mfuasi katika mtandao kuwa "unamwona", amenyamaza sana au wataka aseme jambo. Ni

njia ya kuchokoza mwenzako katika jamii ya mtandao. Mara nyingi katika maisha yakila siku watu huweza kuwasiliana kwa ishara za mwili kama vile kusinziliana macho,kukunjiana uso na kadhalika. Tabia hii hujitokeza katika utangamano wa mitandao ya kijamii kwa kutumia kidokozi ambacho hutumia ishara ya kidole.

### 2.1.14 BANDIKA/GADISHA

Hii ni tafsiri ya "Tag."Kugadisha ni kubandika picha au kiungo katika ukuta wa mtumiaji wa *facebook* au *twitte*r. Sifa hii imetumiwa vibaya ambapo watu walio na nia mbaya hubandika picha punjufu au ponografia katika kuta za watumiaji, swala ambalo huathiri uhusiano wa mtu katika jumuia ya mtandao kwa sababu huonekana kama amepotoka kimaadili.

### 2.1.15 PAKUA NA PAKIA

Kupakua ni kutoa kiungo fulani kutoka kwa mtandao hadi kwa mashine unayoitumia kama vile simu au tarakilishi na kuhifadhi huko. Ni *downloading* katika lugha ya Kiingereza. Si lazima kihifadhiwe katika simu au tarakilihi bali kinaweza kuhifadhiwa katika disketi, diski ama kwa kadi ya kumbukumbu (*memory card).* Kuweka picha au kiungo chochote katika mtandao hasa katika umbo la mtumiaji wa mtandao ni kupakia (*to upload).*

Hizi ni baadhi ya istilahi tu muhimu katika mitandao ya kijamii ambazo zimebuniwa hivi karibuni kukidhi mahitaji ya watumiaji wa mitandao hii ingawa nyingi hasa katika *tweeter* hazijatafsiriwa. Istilahi hizi tutatazirejelea sana katika utafiti wetu.

## 2.2 MAELEZO YA VIJENZI MUHIMU VYA MADA NA UHUSIANO WAKE NA MITANDAO YA KIJAMII

### 2.2.1 MAANA.

Massamba D.P.B (1994) anasema ni kile ambacho neno au tungo huashiria kutokana na dhana, matumizi au kitajwa. Tuki (1990) nao wanasema fahiwa ya neno au kirai kutokana ama na dhana, matumizi au kitajwa. Ishara mbalimbali za kisarufi huweza kuwasilisha maana kadha. Ferdinand de Saussure alieleza lugha kama mfumo wa ishara. Ishara ambazo alisema kuwa huwa ni kiashiria na kiashiriwa. Ishara moja inaweza kusimamia dhana ambayo ni kiashiria na kinachotajwa na dhana hiyo ambacho ni kiashiriwa. Kwa mfano maelezo haya ya maana, yanarejelea maana katika vitengo vitatu.

Vitengo hivi ni:

1. Kitengo cha dhana au kiashiria kwa mfano ishara "fisi."
2. Kitengo cha kitajwa ambacho ni kiashiriwa kwa mfano kiashiriwa cha hapo juu ni mnyama mwenye sifa fulani moja wapo ya sifa hizo ikiwa ni ulafi.
3. Kitengo cha matumizi. Hiki ni kitengo cha matumizi ya ishara fulani.

Ishara inaeleweka katika muktadha maalum kwa mfano katika sentensi.

(a)Hatukumwalika Musa kwa karamu kwa sababu ni fisi.

(b)Mbuzi wa Musa alililiwa na fisi.

Ishara "fisi" katika sentensi (a) imewekwa katika matumizi kuashiria dhana ya ulafi lakini katika sentensi ya (b) ishara hiyo imetumika kuashiria mnyama alaye wengine na ambaye ni mlafi. Mweri J.G (2010) anasema katika kuelewa maana ya tungo

fulani ni muhimu kuelewa yale ambayo mzungumzaji au mwandishi anamaanisha, ni muhimu kufahamu si tu maana ya maneno bali pia kile mzungungumzaji au mwandishi anatarajia kuwasilisha.

Mweri anasisitiza wazo hili kwa sababu mtu anaweza kusema kitu fulani huku akimaanisha kingine katika hali anazua maana ya msemaji. Habwe J. na Karanja P (2004) wanasema maana ya umaanisho inayoshughulikiwa katika kitengo cha Pragmatiki ni maana ambapo mtu husema kitu na kumaanisha kingine. Grice G (1975) anasema maana umaanisho hutokana na msemaji kutofuata kanuni za ushirikiano. Katika hali hii msemaji anazua maana za ziada bali na maana zinazotokana na maana asilia za vipashio katika kauli ya msemaji. Maelezo haja yanaonyesha kuwa maana za maneno katika mazungumzo na muktadha wa matumizi huandamana kwa sababu neno fulani haliwezi kutumika bila kulenga muktadha mahususi wa matumizi. Angalia *tweet (*usemi) ifuatayo kwa mfano hata kama msomaji huenda anaelewa lugha ya Kiswahili vizuri anaweza kushindwa kuelewa maana yake bila kuelewa muktadha wa matumizi. Usemi huu wa Makena Purity ulikuwa unarejelea kauli ya rais wa Kenya akiwasuta na kuwakejeli viongozi wa upinzani, kauli iliyotafsiriwa kuwa nyama ni uporaji wa mali umma. Jambo hili lilipelekea wananchi kumwaga ghadhabu yao kwa rais katika mitandao ya kijamii.




### 2.2.2 USEMI

Massamba D.P.B (1994) anasema, usemi ni kauli itolewayo na mtu ikiwa ama ni neno moja au kirai kimoja, kishazi kimoja, sentensi moja au zaidi.

Tuki (1990) wanasema usemi ni matini ambayo hutoa kitu kamili hasa matini yanayotolewa na mtu mmoja katika mfululizo wa usemaji.

Mweri G. (2010) naye anauita tamko na kusema kuwa ni kile kinachosemwa na mtu mmoja kabla au baada ya mtu mwingine kuongea.

Kulingana na maelezo haya usemi ni tamko au maneno yanayotolewa na mtu fulani ama kwa katika maandishi au kwa mdomo yanayowakilisha maoni au fikra za msemaji au mwandishi kuhusiana na jambo fulani.

Katika mitandao ya kijamii kwa mfano mtu huulizwa, “Unafikiria nini?” Ambapo huandika kilicho katika fikra zake au kilicho mawazoni.  Angalia kauli ifuatayo ya mtumiaji mmoja wa *facebook* **Judith Kathure** ambayo inatolewamaoni na mtumiaji mwingine wa mtandao huo huo.

- 

  **Judith Kathure**

  **My! anaresembls u,his he ua bro?! ungekuwa in a position to read this. . .huh!** (Mchumba wangu anafanana nawe, kwani ni ndugu yako? Nashangaa kama utafikiwa na hili)**(usemi kabla ya wengine kusema/kauli ya kwanza)**Imenipendeza · · Dakika 15 zilizopitavia (kupitia)rununu: ·

  - Mike Kubai amependezwa na hii.

    - 

      Mike Kubai He rily not in a position 2.(Kweli hawezi kufikiwa na ujumbe huu)

    - 

      Judith Kathure Sure mike. .we blocked each othas contacts..(Kweli ni kama tulizuiana kuwasiliana katika mtandao)


      Mike Kubai N i knew it bcz i know 'them'. (Nilikuwa najua kwa sababu najua tabia zao)

    - 

Judith Kathure Hehe!u r craziest.(kicheko! Wewe ndiye wazimu zaidi)

▪ 

Mike Kubai Am not, av neva bn n am sure i wont. Am saying the truth.(Mimi si wazimu na sikuwa wala sitakuwa wazimu. Naongea ukweli)




kutoka kwa http://www.facebook.com/judith kathure

Hapa kuna usemi asilia wa Judith Kathure mtumiaji wa *facebook* ambaye ameona mtu anayefanana na mchumba wake. Anadhani kuwa pengine ni ndugu ya mchumba wake. Kulingana na mdahalo huu ni dhahiri kwamba aliyeonekana ni ndugu yake mchumba wa Judith Kathure.

### 2.2.3. MAZUNGUMZO

Tuki (1990) na Massamba D.P.B (1994) wanasema mazungumzo ni utaratibu wa kuongea baina ya pande mbili. Mazumungumzo tunaweza kusema kuwa ni namna ya pande mbili kutoa kauli kila mmoja wakati wake. Kwa hiyo lazima kuwe na kauli mbili zinazofuatana na ambazo zimetolewa na nafsi tofauti kwa sababu kuna uzungumzi nafsi. Mitandao ya kijamii huhusisha aina fulani ya mazungumzo ingawa ni ya kimaandishi. Tunasema ni mazungumzo kwa sababu kuna hali ya kujadiliana baina ya wahusika. Kwa mfano baada ya usemi wa kathure hapo juu, kinachotokea ni mazungumzo katika mitandao ya kijamii huwa na sifa mbalimbali ambazo huifanya kuwa mfano mmoja wa diskosi. Mitandao ya kijamii ni kama jukwaa ambalo watu

mbalimbali huleta mijadala kadha ili kujadiliwa. Mijadala hiyo huweza kuwa ya kisiasa (diskosi za kisiasa), kidini (diskosi za kidini), au maswala mengine yoyote ya kijamii.

De Beaugrande na Dressler (1981) wanatoa sifa sita ambazo ni muhimu ili kazi fulani ifaulu kuwadiskosi;

a) **Mshikamano wa kisarufi/upatano wa kisarufi** (*cohesion).*

Vipashio vyote katika sentensi lazima vipatane kisarufi ili sentensi zinazotumika katika mazungumzo hayo ziweze kufasiriwa vyema au kuleta maana. Kimsingi lazima kauli zipatane kinjeo, wingi, umoja na kadhalika. Hali hii hudhibitiwa sana katika mitandao ya kijamii na pale ambapo haizingatiwi maana haijitokezi na hadhira lengwa hulalamika.

Utata katika maandishi au mazungumzo hutokana na ukosefu wa mchukuano au upatano katika maaandishi. Kauli huweza kueleweka kulingana na muktadha kwa mfano maandishi yafuatayo katika barabara yasipofasiriwa kimuktadha maana haiwezi kueleweka.

**PUNGUZA MWENDO!!!**

**WAJENZI!!!**

Maandishi haya yanaeleweka katika muktadha wa madereva kwamba anaonywa kutoendesha gari kwa kasi kwa sababu barabara inatengenezwa na si kwamba anaombwa kujiunga na wafanya kazi. Vilevile wasafiri hawawezi kuelewa kwamba wanaombwa kupumzika kwa sababu kalingana na uelewa awali uliopo ni kwamba ujumbe huo ni wa waendeshaji wa magari tu. Kulingana na De Beaugrande na

Dressler (1981) kuna vipengele vitano ambavyo hudumisha upatano katika matini inayotarajiwa kuwa na sifa za diskosi.

**i)** Ubadilishaji**.**

Katika kuakikisha upatano wa vipashio na mfululizo mzuri wa maandishi katika matini ni muhimu kujizuia kurudiarudia neno moja katika sentensi au aya moja. Msemaji hufanya hivi kwa kutumia vibadala au viwakilishi vya nomino katika sentensi au aya. Ubadilishaji unaweza kuhusu nomino, virai au vishazi.

**Lucy Kendi Miriti**

**ulimi haina backbone, inaweza jenga, na inaweza bomoa, be careful, there is power in the tongue (**Ulimi hauna mifupa lakini unaweza kujenga na kubomoa kwa hiyo kuwa makini unavyotumia ulimi kwa sababu una nguvu)

Like · · 53 minutes ago via mobile ·

- 2 people like this.

Neno ulimi linabadilishwa kwa kiambishi cha ngeli –u- ili kuzuia kulirudiarudia.

kutoka http://www.facebook.com/lucy kendi miriti.

ii) Udondoshaji*(ellipsis)*

Pia huchangia katika kuendeleza upatano wa mawasiliano katika matini. Baadhi ya maneno katika usemaji au maandishi hudondoshwa bila kuathiri maana. Ni sawa na ubadilishaji isipokuwa katika udondoaji nafasi ya neno lilidondolewa huachwa tupu. Hii ni sifa inayopatikana sana katika mitandao ya kijamii. Kwa mfano katika http://www.facebook.com/mwenda.

**Kimathi Mwenda** Nairobi mimi huyu.

dakika 45 zilizopita Kupitia rununu.

**Judy Ruth:** kwani ulikuja lini?

**Kimathi Mwenda**: Leo

Hapa neno Nairobi katika swali la msomaji Mwenda limedondolewa. Pia jibu la Kimathi Mwenda lingekuwa "Nimekuja Nairobi leo" lakini anasema tu "Leo". Huu ni udondoshaji katika mazungumzo.

iii) Urejelezi

Pia urejelezi ni njia nyingine inayotumika kuleta upatano katika maandishi. Hapa kipashio cha kiisimu kinadokeza juu ya kipashio kiingine kilichotangulia katika mazungumzo au matini fulani.

Kwa mfano.

Musa : Unaionaye nyumba yangu?

Hemed : Ni nzuri tu, ni aina **ambayo** ningependa kununua hivi karibuni. (Kirejeshi

**ambayo** kinatumiwa kurejelea nomino nyumba)

(iv) Uunganishaji.

Husaidia katika kuleta upatano wa mazungumzo katika matini au maandishi. Uunganishaji huakikisha kuwa kuna uhusiano baina ya vipashio katika matini au maandishi. Ni mbinu inayochangia katika kuleta muumano baina ya vipengele mbalimbali vya matini fulani. Uunganishaji hufanywa kwa kutumia viunganishi kama vile lakini, angalau,hata hivyo na kadhalika.

V) Uhusiano wa kileksika

Katika matini kuna kundi la maneno ambalo hubeba maana. Makundi haya ni nomino, vitenzi na vivumishi. Kuna maneno katika lugha ambayo yanahusiana na kila neno. Neno moja linapotumika msomaji anatarajia aina fulani ya neno kufuata. Kwa mfano pengo katika sentensi hapa chini linaweza kujazwa na namna fulani ya nomino na haiwezi kujazwa na nomino kama vile kiti, jiwe au nguo. Kwa mfano katika kauli hapa chini;

Nilikula --- saa moja asubuhi.

Ni dhahiri kwamba neno linaloweza kujaza pengo katika kauli hapo juu, lazima liwe linarejelea chakula au linatoa taarifa kuhusu kitenzi kula. Maneno katika mitandao ya kijamii hutumiwa kama yanavyohusiana kileksia. Kwa hivyo mwandishi anafahamu visawe, antonimu, haiponimia, homonimia na kadhalika ili kutumia maneno kama yanavyohusiana

b) **Mchukuano (**Coherence)

Kauli za kila msemaji lazima zichukuane kiusababishi. Kila usemi wa mshiriki katika mazungumzo lazima uwe na mantiki. Lazima anayefuata mazungumzo hayo aweze kuelewa chanzo cha kila kauli inayosemwa. Kwa misingi hiyo,katika mitandao ya kijamii mazungumzo katika kurasa za wasemaji lazima yafuatane kiusababishi. Angalia mazungumzo yafuatayo jinsi yanavyotiririka kimantiki.

**Kenzo Genge:** Adolescence hangovers zinasumbua.hae skul kids.(Athari za ujana bado zinasumbua.watoto wa shule)

**Zeck Mula:** umeongea sasa.

**Eliato Mugambi:** ume*score*liwa ama?(umepatwa na kashfa ama kuna shida gani?)

**Mugambi kaloeo:** *True*(kweli)

**Lincy wawira:** *Me am mr than f***d up.they feel like they own the world*.(mimi hata wamenisumbua zaidi.wanaringa sana hawa wanafunzi)

**Kanze Genge:** *True* wa2.(Ukweli marafiki)

Kutoka kwa www.facebook.com/Kenzo Genge saa saba tarehe 17/08/2012.

c) **Kusudi/Dhamira** (intent)

Sifa nyingine kulingana na Beaugrande ni **Kusudi/Dhamira (intent)** Ujumbe katika diskosi lazima upitishwe kwa hiari na kwa lengo fulani au kwa dhamira fulani. Diskosi katika mitandao ya kijamii huweza kuwa ya kisiasa, kidini, kibiashara na kadhalika. Kwa hiyo dhamira ya mazungumzo huweza kuwa ya kibiashara, kisiasa au kidini. Angalia mfano wa kauli iliyo na kusudi la kisiasa kutoka mtandao wa *twitter.*

***Anyang' Nyong'o @AnyangNyongo***

*Even after independence* ***#Kisumu*** *was the 1st town to have a woman elected MP as well as a woman mayor, Madam Grace Onyango "nyar Bungu"*

(Hata baada ya uhuru mji wa Kisumu ndio ulikuwa mji wa kwanza kuchagua mjumbe mwanamke na pia meya, Bi.Grace Onyango, Msichana wa Nyumbani) Kusudi la kauli hii ni kusifu mji wa Kisumu kwa manufaa ya kisiasa.

d) **Ukubalifu** (acceptability)

Lazima hadhira iidhinishe ujumbe utakaotolewa au utakaopitishwa katika mazungumzo ili kuwa diskosi. Kama ni ujumbe wa kisiasa lazima hadhira ikubali kuendelea na mazungumzo kwa sababu mazungumzo si kubishana. Hadhira katika mitandao ya kijamii huweza kutokubaliana na kauli ambazo ni pujufu au zinaudhi kwa sababu zinabeba maudhui chafu au yanaenda kinyume na matarajio ya wengi.

***Mohammed Ali @MohaJichoPevu***

*A Top senior officer is now threatening Robert Alai using the police. Im told that Robert Alai has*

*been summoned at the PPO's office.(*Mtumishi wa serikali aliye na cheo cha juu anatisha Robert Alai kwa kutumia polisi. Nimeambiwa Robert Alai ameamrishwa kufika katika ofisi ya mkuu wa polisi*)*Ni dhahiri kwamba hali kama hii haikubaliwi katika jamii ya msemaji na kwa sababu hiyo si swala la mjadala au la kuzungumzia bali ni kuliacha tu na kukashfu aliye na tabia hiyo.

**d) Taarifa** (informative)

Ujumbe katika diskosi vilevile lazima uwe na **taarifa** mpya**.** Lazima kuwe na taarifa mpya inayopatikana katika mazungumzo ili iweze kuwa diskosi. Mitandao ya kijamii hasa *facebook* na *twitter* huwa na ujumbe au taarifa ambayo hulenga kupitishwa kwa watumiaji.

5m**Kenya Red Cross @KenyaRedCross**

WARNING Heavy Fog along Naivasha - Nakuru highway ZERO Visibility **#Roadsafety**

(Onyo: Ukungu mzito katika barabara kuu ya Naivasha kwenda Nakuru, ni giza totoro)

**Expand Collapse** Reply: ukurasa wa twitter (http://www.twitter.com/Kenya Red Cross @KenyaRedCross**#Roadsafety** (Ijumaa tarehe17/08/2012 saa tisa jioni.

Bila shaka *tweet* hii katika ukurasa wa shirika la msalaba mwekundu ina habari mpya kwa watumiaji wa mtandao wa *twitter*.

f)**Muktadha** (Situationality**)**

Mazungumzo vilevile lazima yajikite katika **muktadha** (Situationality**)**. Kauli zinazotolewa katika mazungumzo lazima ziwe na uhusiano na muktadha wa mazungumzo. Yanayosemwa yasiwe kando ya shughuli za wakati huo. Wakati na njeo huwa muhimu sana katika mitandao ya kijamii. Mazungumzo katika *facebook* na *twitter* huzingatia sana swala la muktadha. Kwa mfano usiku takriban kila mtumiaji wa mitandao hii huwa anatakia wenzake usiku mwema.

Na asubuhi vilevile ni kujuliana hali. Vipindi na majira pia ni muhimu kwa mfano wakati wa

Sherehe mbalimbali watumiaji wa mitandao ya kijamii hujikita katika mazungumzo yanayohusu shughuli hizo. Mazungumzo hapa chini yanahusiana na kupigwa marufuku kwa masomo ya ziada wakati wa likizo, mjadala na hoja zinazotolewa zote zinahusiana na mada hiyo tu na wakati mahususi tu.

1. **Mwenda Patrick Laibuta**

    Jumatano kupitia rununu:15/08/201

    Mutula na Kiilu ni wanaume shule zote igembe south closed (Mutula na Kiilu wanaogopwa kweli shule zote wilaya ya Igembe kusini zimefungwa.)

    Imenipendeza Hainipendezi tena · · Sambaza

Edd Ntongs Hata nyi mmefunga? Wah mambo biadest!(Hata nyinyi mmefunga? Hali ni mbaya sana!)

Jumatano saa 5:54 mchana/ jioni via rununu · ImenipendezaHainipendezi tena

- 

Karithi James sasa hiyo ni furaha kwako?

Jumatano saa 6:20 mchana/ jioni via (kupitia) rununu · Imenipendeza Hainipendezi tena

- 

**Mutabari Ikiao Samuel** Relax at home na akina Tosh.u'v done ua part (pumuzika nyumbani na akina Tosh. wewe umefanya kazi yako)Jumatano saa 7:06 mchana/ jioni kupitia rununu

Kutoka kwa http://m.facebook.com/story.php?story_fbid=478263618868863

Tischer na wengine (2000) wanasema kuwa sifa mbili za mwanzo ambazo ni upatano na mchukuano zinahusiana na matini yenyewe lakini zingine zinashughulikia matini pamoja na muktadha wa msomaji na mwandishi. Swala la muktadha ni muhimu ili kupata maana ya matini hii ndio sababu sifa nyingi zinashughulikia maswala yaliyo nje ya matini.

Matini na muktadha wake kwa hiyo ni muhimu katika mitandao ya kijamii kwa sababu watumiaji wa mitandao ya kijamii hawawasiliani kwa kutumia maneno katika upweke wake bali maneno yanahusishwa na muktadha wa matini iliyoandikwa/sasisho la mtumiaji ili wasomaji waelewe.

Kutegemea muktadha wa hali fulani katika umbo la mtumiaji wa mitandao ya kijamii, msomaji huweza kuelewa kama hali hiyo inadhamiria kutoa taarifa, tahadhari au ni mzaha uliolenga kuburundisha tu.

Kwa mfano kila moja ya kauli hizi ina ujumbe maalum na ina kusudi maalum kutegemea muktadha wa maneno yaliyotumika.

***Morris Da Superboy Murithi***

*Hae brathas en sisters urgin ma4th wachop vinare. 2 kip de fire burning*

*Tumashame mutula*(Salamu ndugu zangu, nawahimiza wanafunzi wa kidato cha nne watie bidii kwa masomo hadi wamwaibishe Mutula)

Sasisho hili linaeleweka katika muktadha wa kipindi cha likizoni na ufahamu wa awali kwamba waziri wa elimu kwa jina Mutula amepiga marufuku elimu ya likizoni. Ni wazi kwamba kulingana na mwenye ukurasa huu waziri anataka wanafunzi waanguke mitihani na kwamba wakitumia likizo yao vizuri na kupita mitihani ya kitaifa watampa soni waziri huyu. Hii basi ni tahadhari kwa wanafunzi wa kidato cha nne.

**Lucy Kendi Miriti**

**Ulimi haina backbone, inaweza jenga, na inaweza bomoa, be careful, there is power**

**in the tongue (**Ulimi hauna mifupa lakini unawez kujenga na kubomoa kwa hiyo kuwa

makini unavyotumia ulimi kwa sababu una nguvu)

Hii ni taarifa inoyotoa funzo.

5m**Kenya Red Cross @KenyaRedCross**

- WARNING Heavy Fog along Naivasha - Nakuru highway ZERO Visibility **#Roadsafety**

(ONYO: Ukungu mzito katika barabara kuu ya Naivasha. Nakuru barabara haionekani. (Ni vigumu kuendesha gari).

Hii ni taarifa inayolenga kutoa tahadhari kwa wasafiri wa magari.

# SURA YA TATU

## 3.0 SIFA ZA LUGHA YA MITANDAO YA KIJAMII KWA JUMLA

## 3.1 MATUMIZI HOLELA YA LUGHA YA KISWAHILI

Lugha katika mitandao ya kijamii ni lugha ya intenenti, kwa hivyo kuna uwezekano wa lugha ya Kiswahili kutumika kiholela. Hii ni kwa sababu lugha ya mawasiliano katika intaneti ni Kiingereza na kwamba ndio lingua franka ulimwenguni kote. Kutokana na sababu hii msamiati mwingi unaohusu teknolojia umetafsiriwa na mwingine kutoholewa moja kwa moja bila kuangalia misingi iliyowekwa katika utohozi huo. Maneno kama vile *apple* (apuleti), *attachment* (kifunge) ,*autocomplete(*kamilisha kiotomati) ,*format*-(fomati).

Haya ni baadhi ya matumizi mabaya ya lugha ya Kiswahili katika uwanja wa teknolojia kwa sababu maneno haya yametoholewa moja kwa moja kutoka kwa lugha ya Kiingereza. Hata hivyo tunacholenga kuchunguza katika sura hii ni matumizi ya lugha ya Kiswahili yasiyozingatia sarufi. Watumiaji wengi wa *facebook* na *twitter* hutumia lugha ya Kiswahili bila kuzingatia sheria zake katika viwango vyote vya lugha. Kwa mfano kiwango cha fonolojia wanatumia sauti za lugha ya Kiswahili kinyume na inavyokubalika. Angalia mfano wa mazungumzo yafuatayo kutoka ukurasa wa mtumiaji wa mtandao wa *facebook* ili kudhibitisha jinsi watumiaji wanavyokiuka sarufi ya lugha ya Kiswahili.

a) **Maina musa**. xaxa ni wakati wa wa2 kufc gava iache kuenjoi Kenyans. (Sasa ni wakati wa

kulazimisha serikali iache kupuuza wakenya)

**ESHER KENDI**: sawaz maina.(Sawa maina)

**Simo mcute:** Mutula aende maina.ama?

**Mary mukamba**:WACHA KU INCITE KENYANS (Wacha kuchochea wakenya) Kutoka http://www.facebook.com/Estherbaariu.

b) Mwandishi alimwendea mamake Salim kumhoji, "unaskia aje baada ya mwanao kuvunja rekodi ya olimpiki." Mama akasema, "tobaa!mwanangu atanimaliza.amevunja sahani zangu, nyungu vikombe. Sasa waniambia kavunja rekodi ya olimpiki. Mimi naomba serikali inisaidie kumlipa olimpiki sababu mie maskini!"

Kutoka ukurasa http://www.facebook.com/vitukouswahili

Ingawa usemi wa kwanza umetumia lugha ya Kiswahili vizuri, uakifishaji wa hali hii unavunja sarufi ya lugha ya Kiswahili (Swala la uakifishaji tutalishughulikia baadaye) Vilevile wanaotoa maoni wanachafua lugha ya Kiswahili kwa jinsi wanavyotumia lugha yenyewe angalia sehemu zilizopigiwa mstari. Kumbuka hatuchambui uchanganyaji wa lugha kama matumizi mabaya ya sarufi ya lugha Kiswahili.

ImenipendezaHainipendezi tena · · Sambaza

Watu 61 wamependezwa

Said Boilerumechokeshwa ni salim umeanza na mamake sasa.(Umechoshwa na Salimu sasa umeanza kumchokoza mamaye?)

Masaa 12 yaliyopita via (Kupitia)rununu · ImenipendezaHainipendezi tena

Wycliffe OtienoHahahaha.(ha!ha!ha!ha!)(Kicheko)

Masaa 12 yaliyopita via(Kupitia) rununu · ImenipendezaHainipendezi tena

Frank Mziray Teh teh teh(Kicheko)

Masaa 12 yaliyopita via (Kupitia) rununu · Imenipendeza Hainipendezi tena

Wilfred Mwawaza Mjomba Hahahaha.Iyo kali aise (Kicheko. Hiyo ni kali aisee!)

Masaa 12 yaliyopita · Imenipendeza Hainipendezi tena

Mohamed Amin Ibrahim Hahahahaha (Kicheko)

Masaa 12 yaliyopita via(Kupitia) rununu · Imenipendeza Hainipendezi tena

Living Tarimo aya banaaa (Mshangao...Bwana!)

Masaa 12 yaliyopita via (Kupitia) rununu · Imenipendeza Hainipendezi tena

Bonnie Musilih kali jo.(Kali bwana)

Masaa 12 yaliyopita via (Kupitia) rununu · ImenipendezaHainipendezi tena

Hezron Kiboko Hahaha silikari shukua hatua(Serikali chukua hatua)

Masaa 12 yaliyopita via (Kupitia) rununu · Imenipendeza Hainipendezi tena

Yusso Said Hemed Buhahahaaaaaaaaa mweh!(Kicheko)

Masaa 12 yaliyopita via(Kupitia) rununu · ImenipendezaHainipendezi tena

Chwor Mon Hahaha kichekeso nayo(Kicheko! Ucheshi huu)

Masaa 12 yaliyopita via (Kupitia) rununu · ImenipendezaHainipendezi tena

Venessa Martroz ahahahahahahaaaa....mbavu sina tena...utashtakiwa kwa kunibunjabunja utanilipia...(Kicheko. Mbavu sina tena...utashtakiwa kwa kunivunjavunja mbavu utanilipa)

Masaa 12 yaliyopita via (Kupitia)rununu · ImenipendezaHainipendezi tena

Miriti Alex Ujinga nayo!!!!!(Ujinga huo!)

Masaa 12 yaliyopita via (Kupitia) rununu · ImenipendezaHainipendezi tena

- 

DonKing Isack Daniel Hahahaha....( Kicheko)

Masaa 12 yaliyopita via (Kupitia) rununu · ImenipendezaHainipendezi tena.

Kutoka http://www.facebook.com/vitukouswahilini

c)baba anauliza, "mulisoma nini leo! "mtoto anajibu, "tulisoma kuwa binadamu wanatoka ukoo wa NYANI",Baba. "dah.. walimu hao.! mwanangu, we uliamini kuwa binadamu tuna ukoo na nyani?"Mtoto anajibu, "ndio, baada ya kukumbuka sura yako!"

Usemi huu vilevile haujazingatia sarufi sahihi ya lugha ya Kiswahili na vilevile wanaotoa maoni

wanatumia lugha ya Kiswahili kinyume na sheria za sarufi yake.

ImenipendezaHainipendezi tena · · Sambaza

Nyagah Stella na wengine 43 wanakipenda hiki.

Neema Simbo Teh!( Tishika)

Masaa 12 yaliyopita via (Kupitia)rununu · ImenipendezaHainipendezi tena

- 


Ali Zaid Waaah..mungu saidia..(Mungu tusaidie katika hali hii)

Masaa 12 yaliyopita via (Kupitia)rununu · ImenipendezaHainipendezi tena

- 

James MikasiMbuyu ana sura kaa ndula yenye viraka vya kupandiliana! (Baba ana sura

mbaya iliyo na madoadoa)

Masaa 12 yaliyopita via (Kupitia) rununu · ImenipendezaHainipendezi tena

- 

Suddy Side Mnyamwezi Bwahahahaaaaa (Kicheko kikubwa)

Masaa 12 yaliyopita via (Kupitia)rununu · ImenipendezaHainipendezi tena

- 

Emma Ayubu Hahahahaha...dah toto jinga xana.(Huyo mtoto mjinga sana)

Masaa 12 yaliyopita · ImenipendezaHainipendezi tena

- 

Mshefa Joseph Kizazi kinapotea sasa

Masaa 12 yaliyopita via (Kupitia)rununu · ImenipendezaHainipendezi tena

- 

Nassir Daddy-cool Nas Hassan duh~!(Lo!)

Masaa 12 yaliyopita · ImenipendezaHainipendezi tena

- 

Miriti Alex Lol!!!!(Lo!)

Masaa 11 yaliyopita via (kupitia) rununu · Imenipendeza Hainipendezi tena

- 

John MwendwaHahaha hatarisha sana(Kicheko.hatari sana)

Masaa 11 yaliyopita via (Kupitia)rununu · ImenipendezaHainipendezi tena

- 

Mussa Hussein Ukistajabu ya musa utaona ya mtoto. (Ukistaajabu ya Musa utayaona ya Firauni) Haya ni Matumizi holela ya methali ya kiswahili.

Masaa 11 yaliyopita via (Kupitia) rununu · ImenipendezaHainipendezi tena

Jackson Mwinga It Cms Fb is Bcoming a gud comercial site 4r some of us here!(Inaonekana *facebook* imetoa nafasi nzuri kwa wengi wetu hapa kuendeleza biashara zao)

Masaa 11 yaliyopita · ImenipendezaHainipendezi tena

- 

Franc Kim Masheu nayo!!!(Ndevu!)

Masaa 11 yaliyopita via (Kupitia)rununu · ImenipendezaHainipendezi tena

- 

Zahoro Godfrey mmmh!(Kuwazia jambo hilo)

Masaa 11 yaliyopita via (Kupitia) rununu · ImenipendezaHainipendezi tena

- 

Florence Mwangi Hahahahahahaha i cn't tek it any mo (Kicheko! Siwezi kuvumilia tena)

Masaa 11 yaliyopita via (Kupitia)rununu · ImenipendezaHainipendezi tena

- 

Anne Waithera hehehe(Kicheko)

Masaa 11 yaliyopita via (kupitia) rununu · ImenipendezaHainipendezi tena

- 

Njue Oscar Usiulize bwoss.( Usiniulize bosi)

Masaa 11 yaliyopita via (kupitia) rununu · ImenipendezaHainipendezi tena

- 

  Balala Amos Lo! Sura ya buda,hata usiseme!(Lo! Sura ya baba,hata usiitaje!)

  Masaa 11 yaliyopita via (Kupitia) rununu · ImenipendezaHainipendezi tena

- 

  Innocent MtuiMtoi mchizi xana.(Mtoto chizi sana)

  Masaa 11 yaliyopita via (Kupitia)rununu · ImenipendezaHainipendezi tena

- 

  Jayceon Crackerdadaaadah!..aki Salim analaana c haba. .Hahaha(Kicheko! Kweli Salim ana laana chungu nzima)

  Masaa 11 yaliyopita via (Kupitia)rununu · ImenipendezaHainipendezi tena

- 

  Young Solja Hahahahahahahahahaha! Huyo mtto bhana anatabu xana(Kicheko.Huyo mtoto anataabu sana)

  Masaa 11 yaliyopita via (Kupitia)rununu · ImenipendezaHainipendezi tena

- 

  Fredrick Makao ha!ha!ha!ha!he!~ (Kicheko)

Katika mijadala hii kuna matumizi mabaya ya fonolojia ya Kiswahili kwa mfano sauti /s/ imebadilishwa na nyengine ambayo haipo katika lugha ya Kiswahili x. Vilevile miundo ya maneno katika mazungumzo haya ina kasoro kwa mfano *sawaz* baadala ya sawa. Swali analouliza mtumiaji "*mutula aende ama?*" Halizingatii sintaksia ya sarufi ya Kiswahili.

Katika mazungumzo haya, ni dhahiri kwamba watumiaji hawa wametumia msamiati ambao ni wao tu wanaoufahamu. Maneno yaliyotumiwa si sanifu na bila shaka yanaishusha hadhi lugha ya Kiswahili. Baadhi ya watumiaji wa mitandao hugundua matumizi haya mabaya ya lugha ya Kiswahili na huelekea kukejeli watu wanaoitumia vibaya kama vile huyu hapa




Tafsiri: Watu wa Laare wamenunuliwa pombe ili wakiona msafara wa gari wapige mayowe. Hata hivyo hilo si tishio mheshimiwa Eruaki ataendelea kuwafanyia wananchi kazi.

Hapa inaeneneka rafikiye ameudhika sana kutokana na matumizi haya mabaya ya lugha ya Kiswahili. Anaona ni kama kuiua lugha yenyewe.

Hili ni jambo hatari kwa sababu wageni na wanafunzi wengi hulenga kujifundisha Kiswahili sanifu kupitia mitandao ya kijamii kama vile *facebook* na *twitter*. Katika hali hii wanajifundisha Kiswahili chapwa. Si wageni tu ambao huweza kueneza matumizi ya maneno yasiyokubalika bali pia wanafunzi na watu wengine wote wanaolenga kujifunza Kiswahili fasaha. Hii ni kwa sababu kadri msamiati mbovu unavyoendelea kutumika katika mitandao ya kijamii ndivyo utapata watumiaji wengi na hivyo kueneza matumizi mabaya ya lugha ya Kiswahili kama moto jangwani.

## 3.2 KUCHANGANYA MSIMBO

Dhana ya uchanganyaji msimbo imeshughulikiwa na wataalam mbalimbali. Bokamba (1989) anasema kuchanganya msimbo ni kuingiza vipashio vya kiisimu kama vile mofimu, neno, kirai na kishazi kwenye vipashio vya viwango vivyo hivyo katika lugha nyingine (tafsiri yetu). Naye Wei (1998) anasema kuchanganya msimbo ni kutumia lugha mbili katika mawasiliano katika kiwango kilicho chini ya kishazi. Pia Massamba D.P.B (1994) anadai kuwa, kuchanganya msimbo ni matumizi ya lugha mbili tofauti kwa mfano Kiingereza na Kiswahili katika muktadha wa mazungumzo au matini moja wakati wa mawasiliano. Buliba A na wengine (2009) wanasema uchanganyaji msimbo ni hali ya msemaji kutumia vipashio au maneno ya lugha mbalimbali katika hali moja ya mazungumzo.

Kulingana na maelezo ya waandishi hawa tunaweza kusema kuwa kuchanganya msimbo ni kutumia sarufi za lugha mbili tofauti katika muktadha mmoja wa

mawasiliano. Ni wazi kwamba mitandao ya kijamii huhitaji matumizi ya tarakilishi, au rununu. Wanaotumia vyombo hivi hasa ni wenye simu zilizo na uwezo wa kutumia huduma za intaneti. Watu hawa lazima wamesoma. Elimu ni njia mojawapo inayosababisha umahiri wa zaidi ya lugha moja na jambo la kuchanganya ndimi katika mawasiliano yao linakuwa la lazima. Umahiri wa lugha nyingi husababisha watumiaji wa mitandao ya kijamii kuwa na uhuru wa kuranda kutoka lugha moja hadi nyingine. Lugha zinazotumiwa mara nyingi huwa ni tatu; lugha ya mama, Kiswahili na lugha nyingine za kigeni kama vile Kiingereza, Kifaranza na kadhalika. Ni nadra sana kupata mtumiaji wa mitandao ya kijamii hasa Afrika ambaye ni monolinguo kwa sababu watumiaji wengi wa mitandao ya kijamii wamepitia katika kiwango fulani cha elimu na kwa hiyo ana uelewa fulani wa lugha mbili au zaidi.

Hata hivyo kuchanganya msimbo kunategemea kiwango cha elimu cha mtumiaji wa mitandao hii pamoja na kiwango cha elimu cha hadhira anayoilenga. Katika mitandao ya kijamii kuna kurasa ambazo huhusu mashirika au makampuni na katika mashirika haya hali ya kuchanganya msimbo ni nadra sana. Hii ni kwa sababu matangazo katika kurasa hizi huwa ni rasmi. Hata hvyo wanasiasa huwa na anwani au kurasa katika mitandao ya kijamii ambazo zinachukuliwa kuwa rasmi lakini wanachanganya msimbo ili kujitambulisha na vijana ambao ndio idadi kubwa ya wapiga kura. Mpaka baina ya sheng na kuchanganya msimbo hasa Afrika Mashariki ni mwembamba mno na kwa sababu hiyo kuchanganya msimbo ni mtindo ambao unapendwa na vijana wengi. Hii ndio sababu viongozi na wanasiasa wengi huchanganya msimbo ili kunata nadhari ya vijana.

Nchini Kenya wanasiasa huchanganya Kiswahili na Kiingereza na wakati mwingine lugha za mama, lakini lugha inayotambulisha mtu binafsi ndiyo huwa inaegemewa zaidi. Hii ni lugha ambayo mtu hujitambulisha nayo katika mazingira yake ya mawasiliano ya kila siku. Angalia *tweet* ifuatayo ya watumiaji wa *tweeter* walio na weledi wa misimbo ya Kiswahili na Kiingereza.

Misingi ya mazingira ya Ken Mananga ni Kiswahili na ya Anyang Nyong ni Kiingereza.

@Ken mananga;Hosting karaoke @SHARLOCK,am telling hii kizungu ni ngumu si ulimi nitaacha ka'pc huku vyenye najiuma??nway your welcome.dakika tano zilizopita 3/7/12.(Nakuambia hii lugha ya Kizungu (akimaanisha kiingereza) inanipa shida mpaka najiuma ulimi)

47m**Anyang' Nyong'o @AnyangNyongo**

*Shukran to all who have sent me messages of support for my***#KisumuFastForward***campaign*

*launching today. I hope to use twitter more.* (pokeeni shukran zangu watu wa Kisumu kwa kuniunga mkono katika uzinduzi wa kampeni zangu)

**Expand Collapse**

3m**Anyang' Nyong'o @AnyangNyongo**

*Even after independence* ***#Kisumu*** *was the 1st town to have a woman elected MP as well as a woman mayor, Madam Grace Onyango "nyar Bungu"* (Hata baada ya uhuru

mji wa Kisumu ndio ulikuwa mji wa kwanza kuchagua mjumbe mwanamke na pia meya, Bi Grace Onyango, Msichana wa Nyumbani.)


Katika bandiko la pili na la tatu, hapo juu ni dhahiri kwamba mtumiaji wa mtandao wa *twitter* anapenda kutumia lugha ya Kiingereza kwa hivyo hata kama anachanganya msimbo, misingi ya mazungumzo yake ni Kiingereza lakini katika bandiko la kwanza mtumiaji ambaye ni mkaazi wa mtaa wa Umoja kule Nairobi ana misingi ya sheng ambayo ni msimbo wenye misingi ya Kiswahili. Pia katika mazungumzo ya mitandao ya kijamii kuna matumizi ya misamiati ya lugha za mama kutegemea anayelengwa katika mawasiliano hayo hasa vyombo vya habari vinavyotumia lugha ya mama katika utangazaji wake. Mazungumzo baina ya mashabiki katika vyombo hivi huchanganya lugha ya mama na lugha zingine kama vile Kiswahili na Kiingereza. Angalia kauli ya tatu ya Anyang Nyong hapo juu *Nyar Bungu* ni maneno ya lugha ya Dholuo ambayo yanatumika pamoja na Kiswahili na Kiingereza.

## 3.3 UFUPISHAJI WA MANENO KATIKA MITANDAO YA KIJMII

Hapa tutaangalia matumizi ya vifupisho au akronimi katika mitandao ya kijamii. Iribemwangi P.I na Mukhwana Ayub (2011) wanasema kuwa, akronimi ni mbinu ya kuchukua herufi za mwanzo kutoka kwa maelezo ili kuunda neno fupi lenye kuwakilisha maelezo husika. Akronimi kwa hiyo tunaweza kusema kuwa ni neno linaoundwa kutokana na herufi au silabi za mwanzo za neno au maneno kwa mfano UKIMWI (ukosefu wa kinga mwilini). Vifupisho vinaweza kutamkika au visitamkike ambapo vitatajwa herufi kwa herufi kwa mfano FB kwa maana ya *facebook.* Watumiaji wa mitandao ya kijamii wamegundua mbinu ya kufupisha neno lolote

kutoka lugha yoyote katika mawasiliano yao maadamu yanataja dhana zinazorejelewa.

Mara nyingi katika mitandao ya kijamii neno au maneno ufupishwa ili kupunguza shughuli za kupiga chapa maneno mengi.  Hii ni kwa sababu watumiaji wa mitandao ya kijamii hutumia simu ambazo zina vitufe vidogo vinavyochosha pia tarakilishi katika mikahawa ya intaneti (cyber café) ambapo malipo yake ni ghali mno.  Pia katika mitandao ya kijamii watumiaji huwa na mfumo mpana wa mtandao wa marafiki na ili kuwasiliana au kupiga ghumzo na wengi iwezekanavyo wanaghundua mbinu ya kufupisha maneno.  Katika usemi huu hapa chini, jina la muungano wa Jamhuri ya Tanzania linafupishwa na kuwa TZ.




Kutoka  www.twitter.com@abelnyalusi

Kupitia mbinu ya ufupishaji wa maneno, vifupisho vingi vya maneno katika mitandao ya kijamii vinatambaa na kufahamika na takriban kila mtu katika jumuia ya *facebook* na *twitter*.  Pia itakumbukwa kwamba baadhi ya mitandao ya kijamii hasa *twitter* huhitajika kuwa na herufi zisizozidi 140, na kwa sababu hiyo watumiaji wa mitandao ya kijamii hubuni sajili ya mitandao ambayo itawasilisha ujumbe kwa maneno machache na herufi chache iwezekanavyo.  Ifuatayo ni orodha ya vifupisho na akronimu maharufu katika mitandao ya *Twitter* na *facebook.*

| AKRONIMU/VIFUPISHO. | MAELEZO YA KIINGEREZA | MAELEZO KATIKA KISWAHILI |
|---|---|---|
| AKA | also known as | Jina liingine hasa la utani/lakabu. |
| Bw | between | Kati ya |
| b/c | because | Kwa sababu |
| Bf | boyfriend | Mpenzi wa kiume. |
| fb | facebook | Facebook |
| F2F | face to face | Ana kwa ana |
| Gb | goodbye | Kwaheri |
| gf | girlfriend | Mpenzi wa kike. |
| HW | home work | Kazi ya nyumbani kwa wanafunzi. |
| OMG | oh my god | Mungu wangu! |
| pliz | please | Tafadhali |
| Qt | cutie | Mtanashati. |
| thx | thanks | Asante |
| Y | why? | Kwa nini? |
| lol | laughing out loud | kicheko kikubwa. |

Hata hivyo akronimi nyingine nyingi zinaendelea kubuniwa kadri siku zinavyoendelea na matumizi yake kupanuka. Angalia baadhi ya matumizi ya vifupisho hivi katika mitandao ya *twitter* na *facebook.*

"**@_shila_m**: do not dial 211 twice you will be charged 2bob per min just to hear a special msg from **@bobcollymore**" ~> Retrieval is free (Kwa Shila_M usipige simu namba 211 mara mbili kwa sababu utalipizwa shilingi mbili kila dakika kusikia sauti maalum kutoka kwa Bobcollymore)

**Expand Collapse**

- 

  Jackson Mwinga It Cms Fb is Bcoming a gud comercial site 4r some of us here!(It

  seems that facebook is becoming a good commercial centre for some of us)

  (Inaonekana*facebook* imeibuka kuwa sehemu nzuri ya baadhi yetu kufanyia biashara)

  Masaa 11 yaliyopita · ImenipendezaHainipendezi tena

  Kutoka kwa htt//www.facebook.com/JacksonMwinga.

Ufupishaji katika mitandao ya kijamii umeibuka na sifa moja ambayo inasisimua. Kila mwanaisimu ambaye atakuwa makini katika mitandao ya kijamii atagundua kuwa maana ya baadhi ya vifupisho katika mitandao ya kijamii ni tofauti na maana ya vifupisho hivyo kama tunavyoifahamu. Mfano mzuri ni kifupisho LOL ambacho ni kifupisho cha maneno katika lugha ya Kiingereza "*laughing out loud*" kwa mfano:




Kutoka kwa htt//www.facebook.com/babayaokevo.

Ingawa sasisho hili ni katika lugha ya Kiswahili anatumia kifupisho hicho kuonyesha ucheshi katika kauli yenyewe.

Haya ni maandishi katika ukurasa wa mtandao wa facebook ambapo kifupisho LOL kimetumika. Tukiangalia katika maandishi haya hakuna jambo linalohitaji kuangua cheko kikubwa. Hii ni kuonyesha kuwa matumizi haya ya kifupisho hichi yamebadilika na kuwa yanaonyesha pengine bahati.

## 3.4 USILABISHAJI KATIKA MITANDAO YA KIJAMII.

Mawasiliano katika mitandao ya kijamii kimsingi huiga mazungumzo ya ana kwa ana. Mitandao ya kijamii ni njia ya watu kufahamiana, kujipatia marafiki na kuendelea kuwasiliana kwa kutumia mtandao wa intaneti. Kwa hiyo wanajenga mfumo wa mtandao wa marafiki na kila wanapokutana mkondoni (online) wanapiga ghumzo kama wanavyopiga katika mazungumzo ya ana kwa ana. Ili kufanikisha mazungumzo haya, watumiaji hubuni mbinu nyingine pamoja na ufupishaji ambayo ni usilabishaji.

Massamba D.P.B (1994) Anasema usilabishaji ni ugawaji wa maneno katika silabi; ugeuzaji wa vitamkwa ambavyo hapo awali havikuwa silabi ili viwe kama silabi. Katika mitandao ya kijamii ugeuzaji wa silabi ni jambo la kawaida sana. Watumiaji wa mitandao ya kijamii hugawa silabi na kugeuza vitamkwa ili vitamkike kwa njia wanayoiona rahisi kutamka. Jambo hili hasa hutokea baina ya watumiaji wa *facebook* na *twitter*.

Katika kufanya hivi watumiaji wa mitandao ya kijamii hutumia herufi na nambari ambazo zinatamkika kwa usilabi wa sauti na maneno wanayoyatumia au wanayolenga

kutumia kuwasiliana. Mara nyingi wanapofanya hivi huchukua sauti kutoka kwa IPA au nambari ili kuleta utamkaji katika sauti au neno lolote wanalolitumia. Wanapofanya usilabishaji; watumiaji wa mitandao ya kijamii huwa hawajali usanifu au usarufi wa lugha wanayotumia. Kilicho muhimu ni kuwasiliana na kupitisha ujumbe au ghumzo na soga katika mazungumzo hayo. Mifano ya usilabishaji imepigiwa mstari katika mazungumzo hapa chini. Vitakwa mbalimbali na maneno vimegeuzwa ili viwe kama silabi kwa lengo la kutamkika kwa urahisi.

- 

  **Khalfan Bamileki teh,teh,teh,,da!sasa kama ndo mwanao anakwambia hivyo cjui unakosaje poz!upo jamaa!(Kicheko,kama mwanako anakwambia hivyo sijui unakosaje raha ipo rafiki yangu!**

Hapa neno linalopitia mchakato huu ni kitenzi "sijui". Katika neno hili mtumiaji wa *facebook* anaamua kupunguza idadi ya herufi katika neno hili kwa kubadilisha silabi 'si' na herufi *C* ambayo katika Kiingereza hutamkwa kama silabi si katika lugha ya Kiswahili.

Masaa 3 yaliyopita via (kupitia) rununu · ImenipendezaHainipendezi tena

Jackson Mwinga It Cms(badala ya *seems)* Fb is Bcoming(badala becoming) a gud comercial site 4r (for)some of us here! )(Ni kama *facebook* imeibuka kuwa sehemu nzuri ya baadhi yetu kufanyia biashara)

Masaa 11 yaliyopita · ImenipendezaHainipendezi tena

**Morris Da Superboy Murithi**

**Hae brathas en sisters urgin ma4th wachop vinare. 2 kip de fire burning tumashame mutula(Hi brothers and sisters am urging you to read and keep the fire burning to ashame Mutula**) (Vipi,ndugu na dada?Nawaomba nyote wanafunzi wa kidato cha nne tusome kwa bidii tumwaibishe Mutula).

Katika hali hii ambapo kuna kuchanganya msimbo kuna usilabishaji kwa mfano

*4th* badala ya *fourth*

*2* badala ya to

*Kip de* badala ya keep the.

**c)hold every one close to ua hrt coz one dei u may wake up n realize that u hv lost diamond while u were busy collecting stones.**(Wapende marafiki au watu ulionao usiwapoteze uking'ang'ania wengine)

ImenipendezaHainipendezi tena · · Masaa 2 yaliyopita

- Watu 4 wamependezwa
-



**Kennedy Muriithi** niajez hilda? may b I wil b busy collectin "GOLD".(Vipi Hilda? Pengine nitakuwa nashughulika na kupata wazuri zaidi)

Masaa 2 yaliyopita via (Kupitia)rununu · ImenipendezaHainipendezi tena


**Pleasant Sherry Stenn** exactly .wewe umeokota nene(Haswa. Pengine wewe umeokota au vipi)

kama saa moja iliyopita · ImenipendezaHainipendezi tena



**Kairithiah Gervas** Dats true hilda.even me ucnibague coz i may b 1 of ur golds. (Hiyo ni kweli Hilda pia nami usinibague huenda nikawa mmoja wa wapenzi wako)

Tukirejelea bandiko hapa chini ukurasa wa 62 tunaona vile mtumiaji wa *facebook* Ramadhan Juma Mohhammed amejaribu kupunguza idadi na urefu wa maneno iwezekanavyo kupitia usilabishaji.


21% 21:04
Hadithi
Ramdani Juma Mohhamed Nilijua waindi wampende m2 mweuc si mchezo awa2pend sisi lakin sisi 2nawapenda wao sisi ni wa2 wema kwao
Dakika 31 zilizopita • Poa• Jibu
Othuman Juma Watu hatari kwa ubaguzi duniani wazungu wahindi waraabu Kama vile hawaendi choo washenzi hao
Saa 1 iliyopita • Poa• Jibu
Amon Lumanyisa nawaunga mkono kwa asilimia miamoja haiwezekani mtu aliyetuita nduli leo unamjengea sanamu la heshima ukiwa na maana kwamba unaunga mkono matamshi yake kwa watu weusi
Saa 1 iliyopita • Poa• Jibu
Andika maoni...

## 3.5 LUGHA KATIKA MITANDAO YA KIJAMII INA SIFA ZA KIKONGAMANO AU MKUTANO DUARA

Mtandao wa kijamii ni kama ukumbi wa mazungumzo ambapo watu hujadili masiala chungu nzima. Katika ukumbi, ambapo watu wengi wanapiga gumzo, mmoja wao hutoa hoja kisha wenzake kuichangia. Kuchangia hoja hutegemea kama kinachosemwa kinakuhusu au la. Ikiwa hoja inayojadiliwa haikuhusu basi hautachangia, vivyo hivyo katika mtandao wa kijamii ikiwa sasisho la mfuasi au rafiki yako katika mtandao wa kijamii halikuhusu basi hutachangia chochote katika mjadala huo.

Kongamano duara ni mkutano wa watu wanaolenga kujadili, kushauriana au kutafuta suluhu kuhusu masiala mbalimbali ambayo huweza kuwa rasmi au ya kawaida tu. Wahusika katika kongamano huweza kuwa wengi au maelfu ya watu. Wahusika katika mitandao ya kijamii ni mfano wa kongamano duara. Marafiki au wafuasi wa mtumiaji wa mtandao wa kijamii ni kama washiriki katika kongamano. Wanaweza kuona na kushiriki kila hoja unayotoa kama sasisho katika ukurasa wako wa *facebook* au *twitter*. Hali hii inaweza kuelezwa kwa kutumia mchoro ufuatao.



Marafiki au wafuasi katika *facebook* au *twitter* wanaweza kuangaliwa kama washiriki wa kongamano. Katika kongamano hilo washiriki wanaoweza kuhusiana au kujadili swala moja wamesimama kwa safu katika mstari mmoja kama inavyoonyeshwa katika mchoro hapo juu. Ni dhahiri kuwa mshiriki mmoja anaweza kuhusiana na wenzake katika zaidi ya safu moja yaani zaidi ya makongamano mawili. Angalia pale mshiriki mmoja anasimama katika makutano ya mistari miwili au zaidi.

Kila mdahalo huhusu yeyote katika kila duara. Kila mhusika anaweza kuwa chanzo cha mdahalo, kwa hiyo mitandao ya kijamii ni mikutano au kongamano duara linalojadili masiala yoyote katika jamii. Ikumbukwe kuwa si lazima kila mtu achangie au atoe maoni katika mjadala hata kama amehudhuria kongamano. Vivyo hivyo katika mtandao wa kijamii si lazima kila mfuasi atoe maoni katika swala la mjadala hata kama ni rafiki au mfuasi. Kongamano au mkutano duara ambao hufanywa na watu walio pamoja au katika kikao kimoja na lugha wanayotumia husheheni sifa za mazungumzo ya ana kwa ana. Jambo hili linaonyesha kuwa sajili ya mitandao ya kijamii ina sifa za mazungumzo ya ana kwa ana. Sifa moja kuu ya lugha ya ana kwa ana ni kuwa wahusika hupata majibu kuhusu swala linalojadiliwa papo kwa hapo na watu huzungumza kwa kupishana zamu. Si kama ilivyo katika barua ambapo mtu huhitaji kusubiri ili kupata jibu. Watu wengi katika mkururo wa marafiki huweza kuchangia na kutoa maoni kama vile katika kongamano la kawaida. Kwa hiyo mtandao wa kijamii ni kama ukumbi wa mazungumzo ambapo gumzo baina ya watu mbalimbali huendeshwa. Ni kama ukumbi wa mazungumzo.

## 3.6 MATUMIZI YA IKONIHISI NA PICHA


Ikonihisi ni tafsiri ya neno laKiingereza *emoticon* ambalo pia linatokana na maneno mawili ya Kiingereza *emotion* na *icon.* Mitandao ya kijamii hutumia ishara fulani zinazowasilisha hisia za uso wa mzungumzaji au msemaji kwa msomaji. Ishara hizi huchukua nafasi za utamkaji na usikivu wa sauti pamoja na ishara zozote za mwili zinazowasilisha ujumbe bila kutumia maneno. Ishara hizi huchukua nafasi ya kunzilia macho, kukunja uso, kuinua mkono na kadhalika. De Saussure alieleza lugha kuwa mfumo wa ishara nasibu, kwa maana kwamba jamii hukubaliana kuhusu maana ya ishara mbalimbali. Kila ishara inapewa maana kulingana na makubaliano ya jamii husika. Kwa mfano jamii ya mitandao ya kijamii imekubaliana katika matumizi ya ishara zifuatazo kuonyesha hisia mbalimbali. Katika kila ishara kuna kisawe chake katika uso halisi. Hata hivyo watumiaji wa mitandao ya kijamii hukubaliana kuhusu kinachorejelewa na ishara hizi. Hapa chini angalia mifano ya ikonihisi zinazotumiwa katika mitandao kadha ya kijamii pamoja na tafsiri yake katika uso halisi.



Mitandao ya kijamii hutumia ishara hizi kwa kiwango kikubwa, hii hulenga kufupisha ujumbe ili kuuwasilisha kwa kutumia nafasi ndogo iwezekanavyo. Ishara hizi huwasilisha hisia mbalimbali kwa mfano furaha, huzuni na kadhalika. Kwa kutumia ikoni hizi rafiki au mfuasi wa mtandao wa kijamii huweza kuwasilisha na kuonyesha hisia mbalimbali kwa njia ya maandishi, hisia ambazo huweza tu kuwasilishwa kupitia mazungumzo ya ana kwa ana. Katika ukurasa wa nyumbani wa *facebook* mtumiaji hukumbana na upau zana ambao huonekana hivi:





Kisha mtumiaji wa *facebook* au *twitter* huchagua mojawapo ya ikonihisi kutegemea hali yake. Ikonhisi huwa na maana mbalimbali kama inavyojitokeza katika maelezo hapa chini.




Imetafsiwa kutoka hpp/www.whapApp.com/725930482.

Katika ukurasa huu mtumiaji wa *facebook* huchagua hali yake kulingana na hisia zake kwa mfano mtumiaji wa mtandao wa *facebook* anayehisi uchovu huchagua ikoni inayobeba ujumbe huo ambapo ukuta wake huwa kama inavyoonekana hapa chini.




Kwa kawaida mtu anapowasiliana kwa lugha ya ana kwa ana, maneno yake huweza kuandamanana ishara za uso, kusinzilia macho, kuinua mikono, na kadhalika. Hali hii huwa haidhihiriki katika lugha andishi kwingineko isipokuwa katika mitandao ya kijamii. Mitandao ya kijamii imeibuka na ishara au picha zinazoonyesha hisia mbalimbali za mtumiaji wa mtandao wa kijamii. Ishara hizi tumeziita ikonihisi katika makala haya.

Ikonihisi zimeenea sana katika mitandao ya kijamii na zimechukua nafasi ya lugha ya maneno kabisa. Mlengwa wa ujumbe katika mitandao ya kijamii anapata ujumbe moja kwa moja. Hii imewezeshwa na maendeleo katika teknolojia ya mawasiliano. Baadhi ya rukono, tabiti, ipadi na tarakilishi huwa na ikoni hizi ambazo hupakuliwa moja kwa moja bila shida yoyote. Hata mitandao ya kijamii kama vile *facebook* na *twitter* ina ikoni hizi katika kurasa zao za nyumbani. Kwa mfano katika ukurasa wa nyumbani wa f*acebook* utapata ikonihisi mbalimbali. Mtumiaji wa mtandao huichagua kutegemea hali yake wakati huo. Wafuasi au marafiki wake wanaweza kupata ujumbe moja kwa moja. Pamoja na ikonihisi ukurasa wa nyumbani wa *facebook* una ikoni nyingine katika upau zana wake ambazo ni pamoja na ikoni ya mahali ulipo kijiografia ambayo huwezeshwa na kifaa cha GPS.

Picha pia hutumika katika mitandao ya kijamii. Matumizi ya picha katika mitandao ya kijamii yamechukua nafasi kubwa sana. Watumiaji wa mitandao ya kijamii huona

rahisi kutumia picha gumzo kuliko kutumia lugha andishi ya maneno. Hii ni kwa sababu kupakua picha ni rahisi. Pia inaburudisha zaidi. Picha huwa rahisi kueleweka kwa hadhira lengwa. Kwa mfano mtumiaji wa mtandao fulani wa kijamii hupendelea kutumia picha kueleza shughuli zao. Baadhi ya mitandao ya kijamii hudhibiti idadi ya herufi zinazotumika katika sasisho moja kwa mfano *twitter* huhitaji mtumiaji kutozidi herufi 144. Kwa sababu hii mashabiki wake hupendelea kutumia picha badala ya lugha ya maandishi ya maneno.




Katika sasisho hapo juu kila mtu anaweza kuelewa kuwa mtumiaji anasema kuwa hana hela za matumizi. Watu wengi huelewa lugha ya picha kuliko lugha ya maandishi. Picha ni lugha bia, kila mtu anaweza kuelewa ujumbe wa picha. Hii ndio sababu wafuasi au marafiki wa mtumiaji wa mtandao wa kijamii anapata maoni

mengi sana kuliko anayesasisha hali kwa kutumia lugha andishi ya maneno. Pia katika matumizi ya picha kuna ujumbe unaopatikana kulingana na picha na umaanisho unaopatikana kulingana na picha hiyo. Mtu anapopakua picha akiwa sako kwa bako na raisi wa Marekani kuna ujumbe kuwa ni raia na rais wake.




Hata hivyo analenga kuonyesha kuwa amefika kiwango cha kutangamana na watu wa hadhi ya juu hasa viongozi kwa hiyo yeye pia ni wa hadhi ya juu. Kwa sababu hii picha zimendelea kuwa jinsi maalum na inayopendwa sana katika lugha ya mitandao ya kijamii, katika jamii ya mtandao picha pia ni njia ya mawasiliano. Hii ndio sababu watumiaji wa mitandao ya kijamii wameifanya mitandao kuwa albamu za kuhifadhi picha zao. Kupitia teknolojia watu huwasiliana kwa kutumia programu ijulikanayo kama gumzo picha (*snapchat)* Hapa mtu hutumia mwenzake picha kisha kudhibiti

mda atakaoweza kuangalia picha hiyo kabla ipotee au ididimie kabisa. Picha hupotea pindi mlengwa anapoiona. Pia lugha ya maandishi huweza kutumia programu hii ya gumzo picha. Kupitia mawasiliano ya picha lugha ya mitandao ya kijamii imeweza kuvuka vizuizi vya lugha kwa kuwa picha ni lugha bia. Katika enzi hizi za utandawazi mitandao ya kijamii imechangia sana katika kufanya ulimwengu kijiji kimoja (Utandawazi).

## 3.8 UAKIFISHAJI KATIKA MITANDAO YA KIJAMII

Uakifishaji ni matumizi ya viakifishi mbalimbali ili kuleta maana fulani inayokusudiwa katika usemi, kauli au mazungumzo. Maana iliyokusudiwa huweza kuwa, kuonyesha hisia fulani kama vile huzuni au furaha, kudadisi kuhusu jambo fulani na kadhalika. Mitandao ya kijamii imeleta mapinduzi makubwa katika matumizi ya alama za kuakifisha katika maandishi na katika matumizi ya lugha kwa jumla. Ni vigumu kuwasiliana bila kutumia viakifishi kwa njia sahihi. Hata hivyo mitandao ya kijamii imebadili kaida zilizozoeleka za uakifishaji kwa kiwango kikubwa.

Baadhi ya viakifishi vimebadilishwa na jamii ya kimtandao na kupewa maana nyingine tofauti na ilivyozoeleka. Viakifishi hivi ni pamoja na nukta, alama za dukuduku, na kiulizi. Pia kuna baadhi ya alama ambazo hapo awali hazikuwa na matumizi mengi katika isimu lakini ustawi katika uwanja wa teknolojia yamezipa umaarufu. Alama hizi ni hashitagi/reli/ngazi(#) na alama ya kwa (@).

Tutachunguza matumizi ya alama hizi tukiangalia namna kila moja inavyotumika katika mitandao ya kijamii. Tukianza na nukta/kitone, matumizi yake

yamebadilishwa na mitandao sana. Kwa kawaida nukta hutumika kuashiria mwisho wa sentensi au mwisho wa kauli au wazo fulani. Hata hivyo mitandao ya kijamii imebadili matumizi ya kiakifishi hiki kwa kiwango kikubwa. Kitone sasa hakitumiwi katika mitandao ya kijamii kuonyesha mwisho wa wazo tu bali hutumiwa kuonyesha jambo linalohudhi/linalokasirisha au kuonyesha uchungu fulani kwa upande wa msemaji. Katika mitandao ya kijamii kitone huja hata baada ya neno moja na pia baina ya maneno mawili ambayo yangeunganishwa na kuwa katika sentensi moja.




(Kutoka kwa www.facebook.com/georgemuroki )

Katika chapisho hili mtumiaji wa *facebook* anatumia nukta baina ya neno moja ambalo kwa kweli haliundi sentensi. Anatumia alama ya nukta kuonyesha kukerwa na kuudhika.

Alama za dukuduku pia ni kiakifishi ambacho kimepitia mabadiliko makubwa. Alama za dukuduku huwa ni vitone vitatu mfululizo. Kwa kawaida alama hizi hutumiwa kuashiria usemi uliokatizwa au usiokamilika. Hata hivyo mitandao ya kijamii inapotumia alama hizi za mdokezo huashiria jambo tofauti kabisa. Watumiaji wa *facebook* hutumia alama hizi kuonyesha kauli iliyotolewa au sasisho ni la mjadala, huonyesha kuwa kauli i wazi kujadiliwa na marafiki wa mtumiaji wa mtandao huo.

Jamii ya mitandao ya kijamii huelewa kuwa inapotumiwa haina maana kuwa kuna kitu au sehemu fulani iliyodondolewa bali huwa mwito kwa wafuasi au marafiki kuchangia hoja hiyo. Wanajua kuwa wanaombwa kutoa maoni yao katika sasisho la mwenzao katika jamii ya kimtandao. Kwa mfano katika sasisho hapa chini, hakuna kilichodondolewa katika swali linaloulizwa. Wafuasi au watumiaji wa *facebook* wanaombwa kutoa mchangowao tu kuhusiana na sasicho hili katika ukuta wa walimu.




Alama ya kiulizi pia imeingizwa katika mitandao ya kijamii kwa kishindo. Kiulizi pia hakijasazwa katika mabadiliko haya. Matumizi ya alama hii ambayo hutumiwa kudadisi au kuuliza swali yamebadilishwa na mitandao ya kijamii. Katika mitandao ya kijamii kiakifishi hiki kinatumika kulalamikia jambo fulani au kupatia dai fulani uzito yaani kusisitiza dai fulani. Vilevile hulenga kuchochea mawazo ya hadhira ambayo ni marafiki au wafuasi wa mtumiaji wa mtandao. Kwa mfano katika sasisho hapa chini hakuna chochote ambacho mtumiaji wa mtandao wa kijamii anataka kufahamu ila anatumia kauli inayotumiwa na wafuasi wa kiongozi wa upinzani nchini Kenya bwana Raila Odinga wakati huo ikiwa kama wimbo wa taifa. Alikuwa akifahamishwa yaliyojiri alipokuwa Marekani kwa muda mrefu. Kwa hiyo Jackie Baibey alikuwa anawachangamsha wafuasi wa kiongozi huyo na si kuuliza swali lolote.




Katika sasisho hili msemaji haulizi swali ila anawachochea marafiki wake kutoa maoni kuhusiana na matendo ya mhubiri fulani.

Kimsingi watumiaji wa mtandao wa *facebook* wametumia alama ulizi kuonyesha kuwa wanayoyazungumzia yamewaingia sana mawazoni.

Alama nyingine ni @ ,alama ya kwa au katika. Kabla ya kuibuka kwa mitandao ya kijamii, alama hii ilikuwa haijitokezi sana katika uakifishaji wa kawaida. Alama hii haikuwa inatumika katika vipashio vya lugha kama vile maneno, vikundi hasa virai na vishazi au katika sentensi. Hata hivyo ilikuwa inatumika katika lugha ya kibiashara au mazungumzo ya kibiashara kutaja bei za bidhaa. Ilianza kutumiwa mnamo mwaka 1971 na Ray Tomlison baada ya kuguduliwa kwa barua pepe ya kwanza. Aliitumia kutaja anwani ya injini tafuti kama vile *yahoo* na *google*. Kwa mfano kiungatim@yahoo.com hii ina maana kiungatim atafutwe katika *yahoo* au kwa *yahoo*. Mitandao ya kijamii hasa *twitter* imeanza kutumia alama hii kwa hali ya juu. Katika mtandao wa *twitter* hutumika kutaja mtumiaji wa mtandao huo kwa mfano



19% 21:09
bbcswahili
#Swahili articles. @bbcswahili
Nyahinga @jjohn0325 11 Sep
@bbcswahili Nigeria kuna mama ana miaka 146 kama sio 156 Ila Kwa vile ni mwafulika uwezi sikia akitangazwa tujalibu kutembea pia africa wapo
M a n u è l @diarraeg 11 Sep
Hivi Makala za #BBCSWAHILI anaandika mzungu anayejifunza kiswahili??kila habari inamapungufu ya kukosea maandishi. #UhakikiWaKazi
1
George Ngasara Yunji @Ngasara 11 Sep
@bbcswahili Hii Korea kasikazini hakuna taifa linaiweza
abel nyalusi @NyalusiAbel 11 Sep
@bbcswahili wa mbeya Tz,kitendo hicho cha Clinton kuwadharau wafuasi wa Donard Trump haoni kama itamgharimu?Wachunge kauli zao

Katika badiko hili alama hii imetumiwa kutaja mtumiaji wa mtandao wa *twitter* ambapo tunapata @bbcswahili kwa maana ya katika ukurasa wa bbc Swahili.

Alama ya reli/hashitagi/ngazi inayoandikwa kama # ni alama nyingine ambayo imepata umaarufu kutokana na ugunduzi na maendeleo ya mitandao ya kijamii. Alama hii hupatikana katika kibodi za tarakilishi, tabiti, ipad na pia rukono. Nchini Kenya, alama hii hujulikana kama hashitagi na kule Tanzania wao huiita alama ya reli au ngazi. Hata hivyo matumizi ya alama hii yamepanuka sana katika ulimwengu wa kidijitali hasa mitandao ya kijamii. Katika mitandao hutumiwa kujumlisha mada ambazo zinabeba ujumbe sawa, unaokaribiana au kuhusiana. Hashitagi huambatishwa mwanzoni mwa neno au kirai bila kuacha uwazi wowote baina ya maneno yanayounda kirai hicho. Kwa mfano #obama au #karibunyumbani. Kwa kutumia alama hii unaweza kupata mada au jumbe zote zinazorejelea Obama au kauli karibu nyumbani katika *twitter* au *facebook.*




Angalia: ujumbe katika vibadiko hapo juu havijatafsiriwa kwa kuwa hauna umuhimu katika sehemu hii. Cha muhimu katika vibadiko hivi ni kuelewa namna hashitagi husaidia katika kujumlisha jumbe nyingi zinazohusiana au zenye mada moja.

# SURA YA NNE

## 4.0. NAFASI YA MITANDAO YA KIJAMII KATIKA KULETA UTANGAMANO, NA KULEGEZA MIPAKA YA KITABAKA KATIKA JAMII

Tunaishi katika dunia mpya ambayo mitandao ya kijamii inatawala. Licha ya kutuunganisha na marafiki zetu muda wote, mitandao ya kijamii hutufanya tufahamu mengi yanayojiri duniani. Watu mbalimbali maarufu kama vile wanasiasa, wanamuziki na kadhalika huitumia ili kufikia mashabiki wao walio mashinani. Mnamo Januari 1/2012 *facebook* ilifikia watumiaji bilioni moja na *twitter* milioni 100. Idadi ikiwa ni ya watu walio na kati ya miaka 17-45 walikuwa na kurasa za kibinafsi katika mitandaohii . Habari kutoka (*http://mashable.com/2012/01/12/facebook_1_bilion_users)*. Watu hutumia mitandao hii katika kupata marafiki, kuendeleza maoni yao, kuwasiliana, kutumiana na kupata picha, video, na sinema baina yao.

Mitandao ya kijamii imechukua nafasi kubwa sana katika uwanja wa mawasiliano. Vijana hasa waliokuwa wanapiga gumzo na kelele kwa mdomo moja kwa moja sasa wamehamisha kelele hizo katika mitandao ya kijamii. Pengine kutokana na maendeleo ya kiteknolojia wananchi katika nchi mbalimbali wameweza kupinga utawala dhalimu kupitia mitandao hii. Mfano wa mataifa hayo ni Misri, Libya na Tunisia walioondoa marais wao mamlakani kupitia uchochezi katika mitandao ya kijamii. Kutoka http://www.thenational.ae/news/facebook-twitter-key-to-Arab-spring-uprisings.

Hawazungumzi kwa njia ya midomo bali ni kupitia maandishi katika mitandao ya kijamii kama *twitter* na *facebook.* Mbinu nyingi za mawasiliano baina ya vijana kama vile huduma za simu, vifaa meme kama vile runinga na radio mabango havitumiki sana. Watumiaji huweza kukwepa mkono wa sheria kupitia kwa mitandao ya kijamii kwa sababu mitandao hii haichunguzwi sana pamoja na uwezo wake wa kutumia majina na anwani bandia (.http://www.smh.com/technology news/can social network overthrow government_2012//

Pamoja na kuleta mapinduzi ya kisiasa, mapinduzi makubwa yaliyoletwa na mitandao ya kijamii ni kupunguza umbali wa masafa baina ya mataifa. Imewasaidia akina yakhe walio katika tabaka la chini kuweza kuwasiliana na wengine walio katika tabaka la juu. Katika maisha ya kawaida viongozi hawawezi kupatikana na kujibu maswali ya umma lakini kupitia mitandao hii wanaweza kuwasiliana na raia wa kawaida. Mfano mzuri ni wa rais wa Nigeria Goodluck Jonathan ambaye alitangaza nia yake ya kuwania Urais katika ukurasa wake wa Mtandao wa *facebook* tarehe 15/09/2010-http://www.facebook.com/Goodluckjonathan. Alitumia mitandao ya kijamii katika kampeni zake na kuwabwaga wapinzani wake kwa kutumia mitandao ya kijamii. Hata baada ya kushinda urais Goodluck aliendelea kuwasiliana na wananchi kupitia mitandao ya kijamii na kujibu takriban kila swali kutoka kwa wananchi.

Kila sasisho la hali la Bwana Jonathan lilipokea maoni milioni moja kwa siku. Aliibuka kuwa kiongozi mwenye wafuasi na marafiki wengi zaidi katika mitandao ya kijamii na kuwashinda kwa umbali viongozi wengine kama vile David Cameron

waziri mkuu wa Uingereza, Chancela wa Ujerumani Angela Markel na rais wa Afrika kusini Jacob Zuma wakiwa pamoja.

Nchini Kenya viongozi wengi wa kisiasa huwasiliana na wapiga kura kwa kutumia mitandao ya kijamii kwa kujibu na kuuliza maswali. Takriban wanasiasa wote maarufu Nchini Kenya wana kurasa za kisiasa katika mitandao ya *facebook* na *twitter* (Mathenge Oliver (Agosti 18, 2012) *politicians invest in ict to reach voter*s.gazeti la jumamosi katika http:/www.nation.co.ke.

Kimsingi mitandao ya kijamii imeweza kulegeza mipaka ya kitabaka katika jamii na kupunguza utukufu uliowatenga viongozi kutoka kwa wananchi kiasi chakushindwa kabisa kutangamana nao. Imeweza kupenya ukuta wa kibwanyenye uliokuwa umewatenganisha na wananchi wa kawaida. Haya ni mapinduzi ya kitabaka kwa sababu wananchi kutoka sehemu mbalimbali wamepata nafasi ya kutangamana na kushiriki katika maswala ya kisiasa ya jamii husika.

## 4.1 HALI YA KUPUUZA KANUNI ZA USHIRIKIANO KATIKA MITANDAO YA KIJAMII

Katika sura ya kwanza, tulishughulikia kanuni za ushirikiano kulingana na **Grice (1975)** ambazo kulingana naye ni muhimu katika mawasiliano (uzungumzaji na usikilizaji). Lengo la sehemu hii ni kuangalia jinsi watumiaji wa mitandao ya kijamii hasa *facebook* na *twitter* wanavyopuuza kanuni hizi katika mawasiliano yao. Kupuuzwa kwa kanuni kulingana na **Grice (1975)** hutokea wakati msemaji anaamua kutofuata mojawapo ya kanuni nne kwa sababu kadha.

**Thomas J (1995)**anasema kuwa mapuuza ya kanuni hutokea wakati msemaji anakosa kufuata kanuni katika kiwango cha usemaji ili kuibua umaanisho.Levinson

.**S.C(1983**) naye anasema msemaji hupuuza kanuni akitarajia kwamba msikilizaji anaweza kufasiri maana nje ya maneno katika usemaji.

Hapa kulingana na Levinson, msemaji hupuuza kanuni akijua kwamba ipo na kwamba msikilizaji atafahamu hivyo na kufasiri maana. Kwa mfano katika mazungumzo hapa baina ya marafiki wawili wa kike A na B, A akimdadisi mwenzake kuhusu mchumba aliyempata hivi karibuni.Anataka kujua ikiwa ana kazi yoyote ama ana kipato chochote.

Msichana A : Hivi uliniambia mchumba wako anafanya kazi gani?

Msichana B : Anaishi Muthaiga hata gari lake ndilo limenileta hapa.

Msichana B hajaonyesha ushirikiano lakini anatarajia kwamba A anaweza kufasiri maana nje ya muktadha wa mazungumzo hayo. Anatarajia kwamba A anajua kwamba mtu anayeishi katika mtaa wa Muthaiga na ambaye ana gari lazima anafanya kazi nzuri. Anatarajia msikilizaji hawe naufahamu awali kwamba mtaa huo ni wa kibwanyenye na wanaoishi huko ni matajiri.Katika muktadha huu kanuni ya uhusiano na kanuni ya idadi zimepuuzwa ili kuibua umaanisho.

Kulingana na Grice msemaji huweza kukosa kuonyesha ushirikiano kwa sababu ya mgongano wa kanuni za ushirikiano. Mgongano wa kanuni huweza kutokea wakati msemaji anaona vigumu kufuata kanuni mbili au zaidi kwa pamoja kwa sababu mbalimbali kwa mfano angalia mazungumzo yafuatayo baina ya mwalimu na mzazi wa wanafunzi wawili waliotumia pesa za karo kununua nguo ambao ni Musa na Abdi.

Mzazi : Mwalimu,unafikiri ni nani alitumia pesa hizo?

Mwalimu : Nafikiri ni Musa au Abdi ingawa hivi karibuni Abdi amekuwa mwanafunzi mzuri sana hata tumempandisha cheo kuwa kiranja katika kidato cha tatu.

Katika mazungumzo haya mwalimu anasema mengi kuliko inavyotarajiwa na pamoja na hayo anakosa kujibu swali. Ni dhahiri mwalimu anasema kuwa Musa ndiye aliyetumia pesa hata hivyo hana uhakika nani aliyetumia pesa hizo na haamini kwamba Abdi angeweza kutumia pesa hizo. Pengine angejibu ni Musa lakini anaogopa kwamba huenda akasema urongo.Kwa hiyo hapa kuna mgongano baina ya kanuni ya idadi na ya ukweli.

Hata kama kanuni hupuuzwa ili kuibua umaanisho, kuna sababu nyingi ambazo hufanya kila kanuni kupuuzwa katika mazungumzo. Si kila wakati mtu anapopuuza kanuni huibua umaanisho. Kwa mfano mtu anaposema urongo na wasikilizaji wake wanakosa kujua kwamba ni urongo hakuna umaanisho unaoibuka ingawa msemaji haonyeshi ushirikiano.

a) **Kupuuzwa kwa kanuni ya ukweli**

Hapa msemaji anatoa kauli ambayo si kweli na ambayo hawezi kudhibitisha.Kuna sababu nyinyi ambazo humfanya msemaji kupuuza kanuni ya ukweli. Mgongano wa kanuni ni sababu moja inayofanya mtu kuvunja kanuni ya ukweli kama tulivyoona katika mazungumzo baina ya mzazi na mwalimu.Msemaji anashindwa kufuata kanuni mbili kwa pamoja kwa mfano anavunja kanuni ya idadi ili kuhifadhi kanuni ya ukweli angalia mfano wa mazungumzo baina ya waziri wa elimu aliyewatetea wanafunzi wa kike waliotaka kuvaa minisketi. (mazungumzo katika lugha ya Kiingereza)

Mwanahabar i: *Did you say girls should wear miniskirts in school Bwana Waziri?*(Je ulisema

wanafunzi katika shule za upili wavae minisketi Bwana waziri?)


Waziri *: No! I didn't say they wear miniskirts. I said they should be smirt and dress as they want*. (La!Sikusema wavae minisketi. Nilisema wawe nadhifu na wavae kama wanavyotaka)

(Kutoka kwa mahojiano baina ya mwandishi wa gazeti la *Daily nation* John Ngirachu ya Jumatatu 23 mwaka 2012, gazeti linalochapishiwa kila siku nchini Kenya)

Hapa waziri haonyeshi ushirikiano kwa sababu hasemi ukweli.Kuna mgongano baina ya kanuni ya ukweli na kanuni ya idadi. Kwa kusema ,"Nilitaka wawe nadhifu," Kisha anaongeza kuwa alitaka wavae kama wanavyotaka, usemi unaopinga kauli ya kwanza kwa sababu inajulikana kwamba wanafunzi walitaka kuvaa minisketi.

Cook(1989) anasema kuwa, kuna uwezekano wa kanuni ya ukweli kupuuzwa bila kusema uongo hata hivyo lazima msikilizaji hawe na uwezo wa kutambua kuwa kanuni hii imepuuzwa. Kulingana na Cook mlengwa anapoelewa kanuni fulani imepuuzwa basi kunakuwa na ushirikiano kwa mfano mwalimu akimwambia mwanafunzi umefanya makosa chungu nzima ama katika Kiingereza mtu anaposema kwamba *I have called you a million times* ni dhahiri kwamba msemaji hajapiga simu mara milioni na haieleweki kwamba amesema uongo bali inaeleweka kwamba ameshirikiana.

Katika mitandao ya kijamii kanuni ya ushirikiano ya ukweli huvunjwa wakati ambapo mtumiaji anasasisha hali yake kwa kutumia kauli au kupitisha ujumbe ambao tunajua

si kweli kwa mfano madai haya ya mtumiaji wa *twitter* kuhusu lugha ya kiswahili ambayo si ya kweli.*22 Aug*  *2012.soft kitty singer @kaygeeuk*

*@SocialBeastie Kiswahili has so few words a lot of them have double meanings so no longer is also never again (intended use of that)* (Lugha ya Kiswahili ina maneno machache kiasi kwamba neno moja linabeba maana nyingi) Kutoka www.twitter.com/kaygeeuk.

*View conversation Hide conversation* (Angalia mazungumzo zaidi) (Maelekezo kutoka kwa mtandao wa *twitter* ambayo tafsiri yake haijatolewa katika mtandao huo)

@SocialBeastie fascinating language 'karibu' is used for welcome, near and come again 'kali' is sharp, fierce & violent - also a hot chilli (Lugha inayovutia kwa sababu ya homonimia zake) @kaygeeuk Sounds good. I had a listen to some Swahili on YouTube. Very fast delivery of words - It must be hard to keep up / comprehend. (Nimesikiliza maneno ya Kiswahili katika youtube yanatamkwa kwa haraka sana kiasi kwamba ni vigumu kuyaelewa)

http://www.twitter.com/socialBeastie

Hata maoni ya wafuasi wake katika mtandao huo yamepuuza kanuni ya ukweli kwa sababu zifuatazo:

(i) Kiswahili hakina upungufu wa maneno/msamiati kama wanavyodai.

(ii) Si kiswahili tu ambacho kina homonimu,lugha nyingi zina maneno yanayotamkwa na kuandikwa sawa lakini yakiwa na maana tofauti.Hili ni tukio la kawaida la kisarufi.

Kulingana na maelezo haya ni wazi kwamba mtumiaji huyu alisasisha hali yake kwa kutumia

kauli ambayo hawezi kuidhibitisha. Mara nyingi kanuni ya ukweli huweza kupuuzwa ili kuzuia kumuudhi mlengwa au msikilizaji kwamfano mazungumzo baina ya mwalimu na mzazi wa mwanafunzi aliyeanguka mtihani wa kidato cha nne.

Mzazi : Alipata alama ya kujiunga na chuo kikuu?

Mwalimu : Ndio! Anaweza kujiunga na mojawapo ya vyuo vikuu vya kibinafsi nchini.

Hapa mwalimu anapuuza kanuni ya ukweli kwa sababu hataki kumuudhi mzazi na katika hali hiyo anapuuza kanuni ya idadi kwa sababu anasema mengi yasiyojibu swali aliloulizwa. Vilevile msemaji huweza kupuuza kanuni kwa lengo la kudhihaki au kukejeli msikilizaji kwa mfano mtoto aliyeacha mifugo kuvamia konde la jirani mzazi anaweza kumwambia, “Ukienda leo pia uwaache ng’ombe waaribu mahindi ya jirani tena.” Hapa anapuuza kanuni ya ukweli ili kuibua umaanisho kwamba anaonywa dhidi ya kurudia kosa alilofanya. Maana huweza kupatikana pengine kulingana na toni katika usemaji. Katika mitandao ya kijamii kanuni ya ukweli huweza kuvunjwa pale mtumiaji anaposasisha hali kwa kusema jambo ambalo wasomaji wanajua si kwaeli. Hata hivyo ni vigumu kujua anachosema si kweli kwa sababu mitandao ya kijamii huwaunganisha watu kutoka sehemu zilizo mbali kimasafa. Kwa hiyo ni vigumu kusema kwamba jambo fulani ni uongo au la pengine kauli inayozungumzia dhana ambayo mtu yeyote anaweza kuifasiri na kuona ukweli ama uongo wake kama hapo juu kuhusu lugha ya Kiswahili.

**(b) Kupuuza kanuni ya idadi**

Kanuni ya idadi huweza kupuuzwa kutokana na msemaji kusema au kutoa habari nyingi au chache kuliko inavyotarajiwa. Msemaji anasema jambo lisilotoa habari

zinazotosheleza mada inayojadiliwa.Hali hii husababisha kuibuka kwa maana nyingine kinyume na ilivyotarajiwa.

Katika mitandao ya kijamii mtumiaji wa *facebook* au *twitter* anaposasisha hali yake hulenga ijadiliwe na itolewe maoni na wafuasi au marafiki wake. Kwa sababu hiyo lazima hiwe na habari zinazotosheleza ili wasomaji waweze kufahamu anachotaka kijadiliwe. Hata hivyo, mengi katika mitandao ya kijamii ni gumzo tu na mara nyingi huwa hayana maudhui bayana. Watumiaji hulenga kuwachochea marafiki ama wafuasi ili wajadili mada yake na ukosefu wa habari kamili za kufafanua mjadala au hali husababisha watu kutoijadili au kuelekea kuuliza maswali mengi kuhusiana na mada hiyo.

Katika takraban kila ukurasa wa mtandao wa kijamii kuna kupuuzwa kwa kanuni ya ushirikiano. Mara nyingi watumiaji husasisha hali kwa kutoa kauli ambazo hazieleweki kikamilifu kwa sababu ya habari finyu zinazojitokeza katika blogu za watumiaji. Hali kama hii inapotokea basi watumiaji huelekea kuuliza maswali ili kufahamu blogu yenyewe kuwasaidia watumiaji kuweza kuijadili kauli hiyo.

Katika hali ifuatayo ya Muthomi Ndurumo mtumiaji wa *facebook*, mjadala uliopo na majibizano yanatokana na mtumiaji huyu kupuuza kanuni ya ushirikiano ya idadi. Anapuuza kutoa habari kamili kuhusiana na ni nani aliyejiua na kwa nini. Hii inasababisha maswali mengi kutoka kwa marafiki zake wa mtandao huu ili wafahamu anachosema. Kadri mjadala unavyoendelea ndivyo watumiaji hawa wa *facebook* wanavyoendelea kuvunja kanuni ya ushirikiano si ya idadi bali uhusiano na hata kanuni ya namna (Kipachiko hapa chini kimehamishwa moja kwa moja kutoka

ukurasa wa mtandao wa *facebook* bila mabadiliko yoyote na kufanyiwa uchambuzi moja kwa moja)

***A REAL MAN.A neghbour of mine who decided to leave the world by jumping at the famous***

***Nyali bridge and went down several metres into the ocean,is the real man.RI*P** (Mwanamme

ambaye ni jirani aliyeamua kuaga dunia kwa kujiangusha katika daraja la nyali na kujiangusha mita nyingi ndani ya bahari ndiye mwanamme kamili. Mungu akurehemu)

Imenipendeza · · Sambaza · Masaa 4 yaliyopita kupitia rununu: ·

Ken Kiecha*Wrong advice*(Mawaidha yanayopotosha)

Masaa 3 yaliyopita · Imenipendeza

Liz Eliza*nyali bridge! ar u joking*?(Daraja la Nyali! Au unacheza?)

Masaa 3 yaliyopita via (Kupitia) rununu · Imenipendeza ·

Muthomi Ndurumo*Ken,can't you recognise the courage of the young man?*(Ken, huwezi kuutambua ujasiri wa kijana huyu?)

Masaa 3 yaliyopita via(Kupitia) rununu · Imenipendeza

Muthomi Ndurumo*Ken,can't you recognise the courage of the young man?Liz,alijitupa huko.Mazishi ilikuwa last week*.( Ken huwezi kuutambua ujasiri wa kijana huyu?Liz mazishi yalikuwa wiki jana)

Masaa 3 yaliyopita via (Kupitia) rununu · Imenipendeza

Liz Eliza N' who is he?(Na ni nani huyo?)

Masaa 3 yaliyopita via (Kupitia) rununu · Imenipendeza

Muthomi Ndurumo*Kajamaa fulani.ntakueleza*(Mtu fulani nitakueleza baadaye)

Anavunja kanuni ya namna kwa sababu hajibu swali la rafiki kama anavyoulizwa, mchango wake hautoshelezi mahitaji ya swali analoulizwa.)

Masaa 3 yaliyopita via(Kupitia)rununu · Imenipendeza

Liz Eliza Sawaz(sawa)

Masaa 3 yaliyopita via(Kupitia)rununu · Imenipendeza

Pam Gal Avd neva heard,then i seem 2 b behide en i liv almost ther.(Sina habari ingawa sijui kwa nini sina habari hiyo na mimi ni jirani yako)

Masaa 3 yaliyopita via(Kupitia) rununu · Imenipendeza

Muthomi Ndurumo Kwani,u r not conversant with yr env(Kwani huelewi yanayoendelea katika kijiji chako?)

Masaa 3 yaliyopita via (Kupitia) rununu · Imenipendeza

Pam Gal I am bur may b tiz bcoz i had concetratd with ma egzams thos 3wks

ago.(Sina habari lakini nafikiri ni vile nilikuwa nashughulika na mitihani wiki tatu zilizopita)

Masaa 3 yaliyopita via(Kupitia) rununu · Imenipendeza

- 

Muthomi Ndurumo Eh! kuna kijana wa kwetu alijitupa Nyali bridge (Naam,kuna kijana wa nyumbani alijiangusha kutoka kwa daraja laNyali)

Masaa 2 yaliyopita via(Kupitia) rununu · Imenipendeza

- 

  Pam Gal Hata hayo ni maendeleo, pengine alizuia mengi tsomi don myd na pole Sana (Hata hayo ni maendeleo, pengine alizuia mkosi mkubwa usijali Muthomi na pole sana kwa msiba)

  Masaa 2 yaliyopita via(Kupitia) rununu · Imenipendeza · 1

- 

  Patrick M'thiruine Nbona anakataa hi tunia na ndivyo iko na mautamuz! (Mbona anakataa kuishi katika dunia hii na jinsi ilivyo na mambo mazuri) kama saa moja iliyopita · Imenipendeza

Kutoka kwa **http://www.facebook.com/Muthomi Ndurumo**

Majibizano katika ukurasa huu yanatokana na hali ya msemaji kupuuza kanuni ya ushirikiano ya idadi. Ni dhahiri kwamba kama angesema moja kwa moja kuna mtu aliyejiua pengine kila rafiki yake katika mtandao angempa pole tu bila maswali mengi. Mapuuza ya kanuni yanasababisha kudadisiwa baadala ya kuliwazwa kwa kumpoteza jirani.

c) **Kupuuza kanuni ya uhusiano**

**Thomas J (1995)**anasema kanuni ya uhusiano hupuuzwa msemaji anapotoa kauli au maoni ambayo hayahusiani na mada inayojadiliwa kwa mfano kubadili mada ghafla. Grice katika **Grundy (2000)**anasemakila usemi au maoni lazima uwe na uhusiano na mada inayojadiliwa wakati huo. Kuwe na uhusiano baina ya maoni yanayotolewa na mada.Kila mchango wa msemaji huwe na uhusiano na mada inayojadiliwa. Naye

**Fregan (2004)** anasemakanuni ya uhusiano inaongoza msemaji kutoa kauli zinazoendanisha na muktadha wa mazungumzo.

Kwa mfano mtu akisema “Lala salama”Jibu litakuwa “Pia nawe” Huu utakuwa ushirikiano katika kiwango cha mazungumzo hayo.

Mitandao ya kijamii huhusu mijadala.Katika mijadala hii watumiaji mara nyingi hutoa hoja ambazo zinapuuza kanuni ya uhusiano ya ushirikiano. Kwa mfano angalia ukurasa ufutao wa mtumiaji wa *facebook*.Hali ya kupuuza kanuni ya uhusiano imeonyeshwa kila inapotokea katika mazungumzo haya.

Maina Kageni · 149,797 wanapenda hii

Masaa 4 yaliyopita saa kumi jioni Jumamosi Agosti 18 2012·

**mpango?**

Imenipendeza · · Sambaza

- Elijah Thuram, Ken Mananga na 77 wengine wanapenda hii.
- 50 kati ya 413
    - 

      Sitindi Manda Mash Lauth Tamasha west (Tamasha katika mtaa wa

      Nairobi West)

      Masaa 2 yaliyopita via(Kupitia) rununu · Imenipendeza

Hajapuuza kanuni ya uhusiano kwa sababu anamwonyesha watakapoenda kujiburudisha.



Pam Kitty hujameez dubai? watch game later(Hujakosa dubai?Katazame

mpira baadaye)

Vilevile maoni yake hayana uhusiano na mada.kwa hivyo anapuuza kanuni ya uhusiano.

Masaa 2 yaliyopita via (Kupitia) rununu · Imenipendeza

- 

Jimmy Rogger Pangoni.

Anapuuza kanuni ya uhusiano.

Masaa 2 yaliyopita · Imenipendeza

- 

Bitter Herb Dottie Njoo saudi.

Mpango wa alasiri moja hauwezi kumfanya kwenda Saudi Arabia kwa hiyo anapuuza kanuni ya uhusiano kwa kufanya kauli kuwa mzaha.

Masaa 2 yaliyopita via (Kupitia) rununu · Imenipendeza

- 

Peter Karachu kuchill at wax.altho nikubiad (Kuendelea na kazi hata kama

Hakuna wateja) Masaa 2 yaliyopita via (kupitia) rununu · Imenipendeza

Huyu pia anapuuza kanuni ya uhusiano kwa sababu anaeleza yanayomhusu bila kushughulikia shida ya mwenye blog


iLavlynn Njokie less…Masaa 2 yaliyopita via (Kupitia) rununu · Imenipendeza

Huyu hata anachokisema hakieleweki, ni dhahiri hakihusiani na mada inayojadiliwa na kwa hiyo anapuuza kanuni ya uhusiano.

- 

  Aaron Tyga Tomatinnho Wa kando Masaa 2 yaliyopita via(Kupitia) rununu · Imenipendeza

Amejibu kuhusiana na neno la msimu maarufu sana nchini Kenya linalomaanisha uasherati. Hata hivyo tunaweza kusema huyu hakupuuza kanuni.Jibu lake limetokana na kwamba aliyeblogi hakufuata kanuni ya idadi na hivyo maana nyingine huweza kuibuka kulingana na wasomaji.

- 

  Imbira Livingston Mabunduki

  Masaa 2 yaliyopita via(Kupitia) rununu · Imenipendeza

Vilevile anavunja kanuni ya uhusiano.

- 

  Danc Wambua bado ma-tym.Masaa 2 yaliyopita via (Kupitia) rununu · Imenipendeza.

Huyu anaonyesha ushirikiano ingawa anaahirisha kumpa maelekezo anayotaka.

Kutoka http:/www.facebook.com/mainakageni

**Aleki Tush.**

**Seemz kila m2 ameenda mafunkie...wenye kudoz gudnit...na cna ucngizi ama niende**

**pia? (**Leo inaonekana kila mtu ameenda sherehe…wanaolala usiku mwema…nami sina

usingizi ama pia niende?)

Katika kusasisha hali mtumiaji wa mtandao huu anapuuza kanuni ya uhusiano anapobadili

mada katika mtandao huo. Hata hivyo anaghundua hivyo na kutumia alama za dukuduku kama kidhibiti usemi.

- Michael Kabarine Kb-Deejay likes this.(imenipendeza)
    -
        - 

          Huxya Mwana Mwema Dennis enda tu usiesabu hasara

          59 minutes ago via mobile ·(dakika 56 zilizopita kupitia rununu)
        - 

          Aleki Tush naona ka nko late budah!(ni kama nimechelewa)

          48 minutes ago via mobile · Like(dakika 48 zilizopita kupitia rununu)
        - 

          Sadie Kiki gdnit 2(usiku mwema pia)-Huyu anavunja kanuni ya idadi na uhusiano.

46 minutes ago via mobile · Like · (Dakika 46 zilizopita kupitia rununu)

- 

Chris Amani kam nikupeleke. beta late dan neva(Kuja nikupeleke bora kuchelewa

kuliko kukosa kufika kabisa)

45 minutes ago via mobile · Like

- 

Judy Ikiara Gnt.(Usiku mwema)


Kanuni ya uhusiano na idadi imevunjwa.

41 minutes ago via (Kupitia) mobile(rununu) ·

Zitah Hannah Gdnt!(Usiku mwema)

Anavunja kanuni ya uhusiaono na idadi.

39 minutes ago via (Kupitia) rununu

- 


Nkirote Peninnah Watoi washaenda, waliobaki ndo we(Watoto wameenda ni sisi tumebaki)

Marafiki wa mtumiaji wa mtandao huu vile vile wanavunja kanuni ya ushirikiano ya Grice hasa wanapomwambia alale salama ilhali amesema hana usingizi na kwamba anafikiria kwenda sherehe pia.

**d) Kupuuza kanuni ya namna**.

**Thomas J (1995)**anasema msemaji kwa hiari hupuuza kanuni ya namna anapokosa kusema au kujibu swali kwa njia inayoeleweka kwa urahisi.kwa mfano mtoto anayelalamika kwa sababu babake ameshindwa kutuliza mgogoro uliopo nyumbani anapoulizwa anasema,"Ningekuwa baba ningechukua msimamo tofauti kuhusiana na mgogoro huo."Mtoto anapuuza kanuni ya namna.Inaibua umaanisho kwamba pengine baba hakufuata utaratibu unaofaa kuhusiana na mgogoro huo. Kanuni ya namna mara nyingi hupuuzwa sana katika maelekezo ya matumizi ya vitu anuwai kama vile vifaa meme kwa mfano rununu, redio na kadhalika. Sheria za kortini na nadharia za kisayansi vilevile hupuuza kanuni ya namna sana.Kimsingi ikiwa mchango wa msemaji unachosha, haueleweki au hauna mpangilio basi haufuati kanuni ya namna.

Katika mitandao ya kijamii watumiaji hupuuza kanuni ya namna ili kuficha siri kwa mfano katika kujadili maswala yanayohusu masiala ya kibinafsi au ambayo kwa sababu fulani msemaji hataki kutangaza hadharani. Katika chapisho la ukurasa wa Muthomi Ndurumo hapo juu, neno *kajamaa* linatumiwakwa kukosa kutaja neno lenyewe la jirani aliyeaga dunia.

# SURA YA TANO

## 5.0 TATHMINI NAMAPENDEKEZO

Tasnifu hii imeshughulikia maana ya usemi na mazungumzo katika mitandao ya kijamii hususan *facebook* na *twitter*. Uchanganuzi huu umezingatia mtazamo wa umaanisho kama ulivyoendelezwa na **Paul Grice(1975)**

Tumeigawa kazi hii katika sura tano. Katika sura ya kwanza tumeshughulikia utangulizi, tatizo la utafiti madhumuni ya utafiti, nadharia tete, sababu za kuchaghua mada, upeo na mipaka, yailiyoandikwa kuhusiana na mada na mbinu za utafiti.

Katika sura ya pili tumeingia katika kueleza istilahi ambazo hupatikana katika mitandao ya kijamii na maneno muhimu katika mada. Hizi ni istilahi ambazo hutumika katika kufafanua na kueleza sura ya mitandao ya kijamii kwa jumla. Tumeshughulikia istilahi kama vile nyumbani, umbo, ukuta, hali na nyingine nyingi. Katika sura hii pia tumeangalia maelezo ya vijenzi muhimu vya mada na uhusiano wake na mitandao ya kijamii.

Sura ya tatu nayo imeshughulikia matumizi holela ya lugha ya Kiswahili, kuchanganya msimbo, ufupishaji wa maneno, usilabishaji, sifa za kikongamano katika mitandao ya kijamii,matumizi ya ikonihisi na picha, na uakifishaji katika mitandao ya kijamii.

Sura ya nne tumeangalia nafasi ya mitandao ya kijamii katika kuleta utangamano na kulegeza mipaka ya kitabaka katika jamii pamoja na hali ya kupuuza kanuni za ushirikiano za Grice katika mitandao ya kijamii.

Sura ya tano inahusu tathmini na mapendekezo, muhtasari wa matokeo, matokeo ya nadharia tete na mapendekezo ya masuala ambayo yanaweza kushughulikiwa na watafiti wa baadaye.

## 5.1 MUHTASARI WA MATOKEO

Utafiti huu umebainisha kuwa lugha katika mitandao ya kijamii ina sifa na majukumu yake maalum. Pia umebainisha kuwa mitandao ya kijamii ina nafasi kubwa katika jamii kwa sababu inawaunganisha watu kutoka matabaka yote katika jamii.

Pia tumegundua kuwa mazungumzo katika mitandao ya kijamii hupuuza kanuni za ushirikiano kulingana na **PaulGrice (1975).** Tumegundua kuwa mojawapo ya sababu za kupuuza kanuni za Grice ni wingi wa watumiaji wa mitandao ya kijamii. Matumizi ya mitandao ya kijamii huhusisha ulimwengu mzima katika mawasiliano na baadhi ya watumiaji huwa hawafahamiani na kwa hiyo kanuni za Grice hupuuzwa ili kuficha siri kwa wasiohusika au kujiepusha na kutoa habari muhimu kwa umma.

Kanuni za Grice za ushirikiano hupuuzwa sana katika mitandao ya kijamii. Hata hivyo, mawasiliano huendelea bila tatizo lolote la kutoelewana.Kwa hiyo ni dhahiri kuwa kanuni za Grice za ushirikiano si muhimu sana katika kuleta maelewano.

### 5.2 KUHUSU NADHARIA TETE

Haipothesia zetu zilikuwa tatu. Kwanza tulichukulia kwamba lugha ya mitandao ya kijamii huwa na sifa maalum ambazo huipa uwezo fulani unaochangia katika kutekeleza majukumu yake. Tumeonyesha vizuri jinsi lugha ya mitandao ya kijamii

inavyosheheni sifa mbalimbali ambazo huchangia katika kufanikisha mawasiliano. Kwa kuzingatia haipothesia hii tumegundua kuwa uchanganyaji msimbo, usilabishaji na sifa zingine tulizozishughulikia husaidia sana katika kuipa lugha ya mitandao ya kijamii upekee fulani unaoifanya kuwa tofauti na sajili nyingine.

Haipothesia ya pili ilidai kuwa, ni lazima muktadha wa usemaji ueleweke ili kupata maana ya kauli au chapisho za mitandao ya kijamii.  Haipothesia hii kulingana na matokeo ya utafiti wetu ina mashiko kwa sababu midahalo katika mitandao ya kijamii hushirikisha watu kutoka mazingira tofauti.  Kwa hiyo ni muhimu kwanza kuelewa anayesasisha hali katika *facebook* au *twitter* anazungumzia nini.  Kuweza kuelewa maana ya msamiati uliotumika katika mitandao ya kijamii pekee si hoja bali pia muktadha wa usemi wenyewe.

Pia tulishikilia katika haipothesia ya tatu kwamba diskosi katika mitandao ya kijamii hufanana kabisa na mazungumzo ya ana kwa ana. Tumegundua kuwa lugha katika mitandao ya kijamii husheheni sifa ambazo haziwezi kutumika katika lugha au mazungumzo ya ana kwa ana.  Sifa hizi ni kama vile matumizi ya vifupisho maalum, usilabishaji na msamiati mwingine unaotumika katika mitandao ya kijamii.  Hizi ni sifa ambazo haziwezi kupatikana katika mazungumzo au mijadala ya ana kwa ana. Hata hivyo kuna sifa za lugha ya ana kwa ana ambazo hupatikana katika lugha ya mitandao ya kijamii kama ishara za mwili na kupishana zamu katika mazungumzo,kwa hiyo haipothesia hii vilevile haina mashiko kwa sababu lugha katika mitandao ya kijamii huchanganya sifa za mazungumzo ya ana kwa ana na pia za lugha andishi. Kwa sababu hiyo haipothesia hii tunaitupilia mbali.

## 5.3 MAPENDEKEZO

Utafiti huu umeshughulikia uchanganuzi wa kiisimu wa lugha katika mitandao ya kijamii kwa kiwango ambacho tunadai kinaridhisha. Hata hivyo hatuwezi kusema kwamba uchunguzi huu umekamilika na kwamba mitandao ya kijamii haiwezi kufanyiwa utafiti mwingine. Baadhi ya istilahi katika *facebook* na *twitter* hazijatafsiriwa. Istilahi hizi zinahitaji kutafitiwa ili kuibuka na tafsiri mwafaka katika lugha ya Kiswahili.

Mitandao ya kijamii inahitaji kufanyiwa utafiti wa kifasihi ili kuchambua maudhui yanayopatikana katika mitandao hii. Mijadala katika mitandao ya kijamii huhusu maudhui mbalimbali kutegemea watumiaji, wakati, na umri wa watumiaji. Vilevile matumizi ya mitandao ya kijamii yamekashfiwa na watu wengi kuhusiana na kupoteza na kupotosha watoto wa shule. Madhara yanayoletwa na mitandao ya kijamii hayajafanyiwa utafiti wa kina. Katika utafiti wetu tumetumia nadharia moja tu; nadharia ya umaanisho kama ilivyoelezwa na Paul **Grice (1975**). Ingawa nadharia hii imeshughulikia maana katika mitandao ya kijamii, uchunguzi zaidi wa kiisimu unaweza kufanywa kwa kutumia nadharia za umuundo ili kuangalia vipengele vingine vya kisarufi kama vile miundo ya sentensi na maneno katika mitandao ya kijamii.

## MAREJELEO


Abdulaziz-Mkilifi, M. (1972). "*Triglossia and Swahili-English bilingualism in Tanzania". Language in Society, I, 197-213*

Austin, J. L. (1962)*How to Do Things With Words*. Cambridge: Harvard UniversityPress.

Beaugrande, Robert de (1991) *Linguistic Theory: The Discourse of Fundamental Works.*London: Longman

Beaugrande, Robert de, na Wolfgang Dressler (1981) *Introduction to Text Linguistics*. London: Longman.

Beaumont, Claudine (Februari 23,2009) *Twitter users send 50 million tweets per Day- Almost 6oo tweets are sent per second.* The daily Telegraph, London. Ilipatikana Juni,18 2009 katika htt://www.telegraph.co.uk/tecknology/twitter/7297 54/

Blommaert, J. (2005). *Discourse*. Cambridge: Cambridge University Press.

Brown, G., and George Yule (1983). *Discourse Analysis*. Cambridge: Cambridge University Press.

Buliba A na wengine (2009) *Isimujamii kwa wanafunzi wa Kiswahili.* Nairobi, JKF.

Brundage,Sandy(Februari 8,2011) *"facebook moving headquarters to Menlopark:socianetworking giant to move into former sun/oracle campus*.TheAlmenacMenlo park,CA.katika http:/www.almananews.com/news/show-story-php[2]id=8270

Carter, R. (1997). *Investigating English Discourse*. London: Routledge.

Cheng,L.&Butler,K.(1989).*Code-switching: A Natural Phenomenon vs. Language"Deficiency"*. World Englishes8(3). 94

Cook.G (1989) *Discourse*. Oxford: Oxford University Press.

Dummett, Michael. Frege(1981) Philosophy of Language, 2nd Edition. Cambridge:Harvard University Press.

Gee, J. P. (2005). *An Introduction to Discourse Analysis: Theory and Method.* London:Routledge.

Githiora, C. (2002). *"Sheng: Peer language, Swahili dialect or emerging Creole?"Journal of African Cultural Studies 15, 2: 159-81*.

Grundy. 2000. *Doing pragmatics.* London: Arnold.

Habwe J na Karanja(2004)*misingi ya sarufi ya Kiswahili,*Nairobi.phoenix publishers ltd.

Huang,Carol(Juni 6,2011) *''Facebook and Twitter key to Arab spring uprisingrevort,''TheNational ilipatikana Julai 7,2012* katika http:/www.thenational.ae/news/

Grice.H.P (1975) "*Logic and conversation*." *ibid*. Reprinted in *Studies in the Way ofWords*, ed. H. P. Grice, pp. 22–40. Cambridge, MA: Harvard University.

Hymes, D. (1962) *The Ethnography in Speaking. In: T. Gladwin (ed.), Anthropology And ManBehaviour.* Washington.

Iribemwangi na Mukhwana Ayub (2011) *Isimujam.* Nairobi, Focus Publishers.

Kamau, S.N. (2005) *Matumizi ya Kiswahili katika Tarakilishi*, Masters Thesis(Unpublished): Kenyatta University.

Khayesi, M.K. (2002*) 'Kiswahili and Information Technology (I.T) : Challenges inPublic University Libraries in Kenya' katika Kiswahili* Juzuu 65 Dar- es - Salaam, .U.K.I. uk. 24 – 31.

Leech.G (1983) *Principles of pragmatics*. London and Newyork.Longhorn.

Levinson.S.C (1983) *Pragmatics.* Cambridge. Cambridge University press

Mathenge Oliver (Agosti 18,2012)*politicians invest in ict to reach voters*.gazeti la jumamosi katika http:/ www.nation.co.ke

Mayeku, P (Desemba 9,2011) *top 10 socialnetworking sites in Kenya.* Ilipatikana Agosti 3,2012katika http:/www.openbook.co.ke/2011//

Mbaabu, I. (1989) *'Ukubalifu wa Msamiati: Mifano kutoka Kenya' katika Makala yaSemina ya Kimataifa ya usanifishaji wa Istilahi za Kiswahili*, Dar-es -Salaam,.U.K.I. uk. 23 – 28.

Mwaringa,D K.(2009) *Globalization and cultural impact of the media:A web analysis of the facebook social network,* Masters Thesis (Unpublished) University of Nairobi.

Mwaro, A.G. (2002) *'Mchango wa A.S.Nabhany katika Utafiti na Utandaridhi waIstilahi za Kiswahili' katika Utafiti wa Kiswahili,* Maseno, MasenoUniversity. Uk 49 – 56.Mweri G (2010) *Utangulizi wa isimu.*Nairobi, KLB.

Nyuyen,Lananh (Aprili 12,2004)" *Online network created by Havard studentsflourishes".*TheTurfs Daily Medford,

MA.ilipatikana Aprili 20, 2012katikahttp:/www.turfsdaily.com/2.5541/online network created by.Havard-studentsflourishes.

Sagolla, Dom(Januari 30,2009) *"How Twitter was born"* 140 Characters. Ilipatikan Julai 14,2012 katika http:/www.140characters.com/2009/01/30/how-twitter-was-born/

Sano,David(Februari 18,2009) *"Twitter creator Jack Dorsey illuminates the site's foundingdocument. Los Angeles Times* ilipatikana Juni 18,2009 katika www.latimeblogs.latimes.com/technology/2009/02/twitter-creator.

Sullivan, T. (1994*) Key Concepts in Communication and Cultural Studies,*Canada, Routledge Press.

Wei, L. (1998). *The 'why' and 'how' questions in the analysis of conversational codeswitching. In P. Auer (Ed.), Code switching in conversation: Language,interaction andidentity* (pp. 156–176). London, UK: Routledge.

Wei, L. (2005). *"How can you tell?" Towards a common sense explanation ofConversational code switching*. *Journal of Pragmatics*, *37*(3), 375–389.

Thomas .J (1995) *Meaning in interaction: An introduction topragmatics.*London. Longhorn.

Tuki (1990) *Kamusi sanifu ya isimu na lugha*.Dar-es-salaam.Educational publishers andstributors Ltd.

Wells,Roy(Agosti 8,2010) *“41.6% of the US population has a facebook account”*Social mediaToday ilipatikana Julai 1,2012 katika ttp:/www.socialmediatoday.com/index.php².9=roy wells1//

ESPN (Julai 8, 2011) “*Women’s world cup finals breaks Twitter record”* ilipatikana Julai 18,2012 katika htt:/esp.go.com/sports/soccer-news/

# WOVUTI ZILIZOTEMBELEWA


*http://www.facebook.com/shoesilike/Kiungatim.*

http://www.funny.org.in/newspaper.php —

http:/*www.standardmedia.co.ke*.

http:/www.facebook.com

http:/www.cp.africa.com

http://mashable.com/2012/01/12/facebook_1_bilion_users

http://smh.com/technology .

http://www.uncp.ed/home/ a Curtis/newsmedia

http://venturebeat.com/2008/12/18-history-and-growth-of-facebook

http://en.wikipedia.org/w/index.php?title=Meaning_(philosophy_of_language)&oldid=50082780

htt:/www.esp.go.com/sports/soccer-news/